# Nipashe

Jumamosi Mei 7, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580938

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital · nipasheTZ · nipasheTZ · nipasheTZ · 0745 700710

LIKE & FOLLOW US



SportPesa

TZS. 1,224,601,040

BET LEO UWE BILIONEA

SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#




**Baba** mwenye nyumba mbaroni kwa tuhuma za kumnajisi mtoto

UKURASA 3



## DYBALA RASMI KUONDOKA JUVENTUS

UKURASA 22

# Sababu Sabaya kushinda rufani

UK. 2

## YALIYOMO

UKURASA WA 4

### AACHIWA HURU BAADA YA MTOTO KUDAI HAKUBAKWA

MAKAHAMA ya Mkoa Wete imeliondoa shauri la kubaka lililokuwa linamkabili Omar Hemed Abdi (23), mkazi wa Kwale Micheweni, baada ya mtoto wa miaka 12 aliyedaiwa kufanyiwa kitendo hicho kukana.

UKURASA WA 4

### MCHAKATO WA EJAT 2021 WAIVA, SAMIA MGENI RASMI

KAZI 598 zimewasilishwa kuwania Tuzo ya Umahiri wa Uandishi wa Habari Tanzania (EJAT) Mwaka 2021, huku Rais Samia Suluhu Hassan akitarajiwa kuwa mgeni rasmi katika utoaji wa tuzo hizo jijini Dar es Salaam Mei 28, mwaka huu.

## LATRA yaruhusu nauli mpya zitumike

UKURASA 2



Aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai, mkoani Kilimanjaro, Lengai Ole Sabaya (katikati), akizungumza na mawakili wake, Moses Mahuna (kushoto) na Fauzia Mustapha, katika Mahakama Kuu Kanda ya Arusha jana, kabla ya kuanza kusikilizwa kwa hukumu ya rufani namba 129 katika kesi ya jinai namba 105, iliyokuwa inamkabili ambapo mahakama hiyo, ilimwachia huru na wenzake. **PICHA: ALLAN ISACK**

## Serikali yafufua majadiliano ujenzi Bandari ya Bagamoyo

UK. 3


**MICHEZO** NABI AMWAGA 'SUMU' YANGA UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6

# LATRA yaruhusu nauli mpya kuanza kutumika

**Na Richard Makore,** MWANZA

MAMLAKA ya Udhibiti wa Usafiri wa Nchi Kavu (LATRA) imeruhusu wamiliki wa magari ya abiria jijini Mwanza (daladala) kuanza kutoza nauli mpya, ikitengua agizo la awali walilotoa la kupandisha nauli kuanzia Mei 14 mwaka huu.

LATRA jijini Mwanza jana ilitangaza kuanza kutumika nauli mpya ambayo ni ongezeko la Sh. 100 kwa kila safari, kinyume cha tangazo lake la awali, lengo likitajwa kuwa ni kuepuka mgomo wa kutoa huduma ya usafiri uliokuwa umepangwa na wamiliki wa daladala kama kusingekuwa na ongezeko la nauli.

Jana asubuhi, gari la matangazo lilipita maeneo mbalimbali ya Jiji la Mwanza na kutoa tangazo la ongezeko la bei kwa usafiri wa daladala.

Akizungumza na Nipashe, mmoja wa maofisa wa LATRA jijini Mwanza ambaye hakutaka kutaja jina lake, alikiri kwamba bila kufanya hivyo, wamiliki wa magari hayo wangegoma kutoa huduma.

Alisema uamuzi wa awali ulikuwa nauli mpya ianze kutumika Mei 14 mwaka huu kwa ongezeko la Sh. 100 kwa kila safari moja ama kituo kimoja hadi kingine.

Hata hivyo, alisema ili kuzuia mgomo huo wa wamiliki wa daladala, walilazimika kutangaza nauli hiyo ianze jana badala ya Mei 14.

Aliongeza kuwa juzi jioni walifanya kikao na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mwanza na kukubaliana kwamba jana watangaze nauli mpya kwa jiji zima.

Alisisitiza kupanda kwa nauli kumetokana na kupanda kwa bei ya mafuta katika mikoa mbalimbali ambayo imesababisha wamiliki wa daladala kulalamika kutaka nauli nayo iongezeke.

Kutokana na hali hiyo, jana asubuhi baadhi ya abiria walilamikia na hata kufikia hatua ya kurushiana maneno na makondakta wa daladala waliotaka kuwalipisha nauli mpya.

Baadhi ya abiria walisema nauli hiyo iliyotangazwa na LATRA, muda wake wa kuanza kutumika ulikuwa bado na kwamba walishangaa jana kuambiwa imepanda.

Hivi karibuni LATRA ilitangaza nauli mpya za mabasi ya mijini, maarufu daladala, na mabasi ya masafa marefu yanayokwenda mikoa mbalimbali nchini.

Akitangaza kiwango hicho kipya cha nauli hiyo Aprili 30 mwaka huu, Mkurugenzi Mkuu wa LATRA, Gilliard Ngewe, alisema kiwango hicho kipya kingeanza kutumika baada ya siku 14.

Alisema kwa mabasi ya mijini kuanzia kilomita 0 hadi 10 nauli itakuwa Sh. 500 badala ya 400 na nauli ya Sh. 450 itakuwa ni 550.




Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba na Balozi wa Norway hapa nchini, Elisabeth Jacobsen, wakionyesha ripoti ya kuelekea kwenye nishati jadidifu nchini yenye kauli mbiu "Kuwezesha Maendeleo Endelevu" inayolenga upatikanaji wa huduma za nishati nafuu na za uhakika ifikapo mwaka 2030 pia kupunguza uzalishaji wa gesi joto kutoka kwenye sekta ya nishati, baada ya kuizindua jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Sababu Sabaya kushinda rufani

**Na Allan Isack**, ARUSHA

MAHAKAMA Kuu Kanda ya Arusha, imemwachia huru aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, Lengai Ole Sabaya, baada ya kuweka bayana kuwa mawakili wa mrufani wa pili na wa tatu hawakupatiwa nafasi ya kuwahoji maswali ya dodoso (cross examination) mashahidi wa shahidi wa pili na wa tatu wa Jamhuri.

Pamoja na kushinda rufani hiyo waliyokata kupinga kifungo cha miaka 30 jela kutokana na kukutwa na hatia katika kesi ya unyang'aji wa kutumia silaha, Sabaya na Sylvester Nyegu wataendelea kusota mahabusu katika Gereza la Kisongo.

Kuendelea kukaa katika gereza hilo kunatokana na kukabiliwa na kesi ya uhujumu uchumi ambayo itatolewa hukumu Mei 31, mwaka huu. Mrufani wa kwanza katika kesi hiyo ni Ole Sabaya wa pili ni Nyegu na wa tatu ni Daniel Mbura ambaye amekwenda nyumbani baada ya hukumu ya jana.

Akisoma hukumu hiyo jana, Jaji wa Mahakama Kuu, Sedekia Kisanya, kutoka Mahakama Kuu Kanda ya Musoma, alisema warufani hawakupewa nafasi ya kuwahoji mashahidi wa pili na watatu wa Jamhuri. Kutokana na kutopewa nafasi hiyo, mawakili hao hawakutendewa haki kama sheria inavyoelekeza.

"Kwa mujibu wa sheria, warufani walitakiwa kuwafanyia maswali ya dodoso shahidi wa pili na wa tatu wa Jamhuri hivyo hawakutendewa haki na mahakama imewaachia huru warufani wote huru labda kama kuna jambo lingine linafanya waendelee kushikiliwa," alisema Jaji Kisanya.

Wakati akisoma hukumu hiyo, alisema waleta rufani hao walishtakiwa kwa makosa matatu ya unyang'anyi kwa kutumia silaha lakini pia kwa kosa la kupora fedha katika duka la Mohamed Al Saad, Sh. milioni 2.769, Jamhuri walishindwa kuthibitisha kuwa fedha hizo zilichukuliwa.

Alisema Jamhuri walipaswa kuthibitisha kuwa fedha hizo zilichukuliwa lakini hawakufanya hivyo, pia ushahidi wa mashahidi wa kwanza, pili, tatu na saba unakinzana kuhusu kuchukuliwa kwa fedha hizo.

Kuhusu hoja ya majina ya mrufani wa tatu yaliyoandikwa katika hati ya mashtaka kuwa siyo halisi kama alivyodai Mbura mahakamani, Jaji alisema Jamhuri wakati wa kufanya upelelezi na kufungua mashtaka walitakiwa kuthibitisha jina kamili la mhusika.

Kabla ya kutolewa kwa hukumu hiyo, katika viwanja vya mahakama, askari na makachero walikuwa wameimarisha ulinzi nje na ndani ya chumba cha mahakama.

Hukumu hiyo, ilianza majira ya saa 50:50 asubuhi hadi saa 7:50 mchana na ilisikilizwa kwa saa mbili hadi kutolewa uamuzi Jaji akipitia hoja 14 zilizowasilishwa na waleta rufani hao, kupinga hukumu iliyotolewa na Mahakama ya Hakimu Mkazi Arusha.

Baada ya kutolewa kwa hukumu hiyo, wafuasi, ndugu, jamaa na marafiki wa warufani hao, waliangua vilio vya furaha kutokana na kufurahia uamuzi uliotolewa na mahakama hiyo.

Mama mzazi na mke wa Sabaya, walibubujikwa machozi ya furaha huku wakipiga magoti kumshukuru Mwenyezi Mungu kutokana na hukumu hiyo ambayo kwa upande wao imeonekana imewafurahisha.

Katika kesi hiyo, Shitaka la kwanza la unyang'anyi wa kutumia silaha, ilidaiwa kuwa Februari 9, 2021, wakiwa Mtaa wa Bondeni, Jijini Arusha, katika duka la Sahiid Store, warufani wote kwa pamoja (wakati huo wakiwa washtakiwa) wakiwa na silaha, walifanikiwa kumpora Bakari Msangi Sh. 390,000 na simu mbili na kabla ya uporaji walimshambulia kwa kumpiga ngumi, mateke, kofi na kumtishia kwa silaha.

Shitaka la pili lilikuwa linawakabili wote kwa pamoja ikidaiwa kwamba Februari 9, 2021, walipora kaunta katika duka la Mohamed Al Saad, Sh. 2,769,000 na kabla ya uporaji waliwapiga, mateke, makofi, na kuwatisha kwa silaha watu waliokuwapo na kuchukua kiasi hicho cha fedha.

Shitaka la tatu lilikuwa la unyang'anyi wa kutumia silaha lililokuwa likiwakabili washitakiwa wote ikidaiwa kuwa Februari 9, 2021, katika Mtaa wa Bondeni Jijini Arusha wakiwa na silaha walipora simu moja ya mkononi aina ya Tecno, Sh. 35,000 mali ya Ramadhani Rashid.

Pia ilidaiwa kuwa kabla ya kufanya uhalifu huo waliwaweka chini ya ulinzi watu wote waliokuwa ndani ya duka la Mohamed Saad.

## Baba mwenye nyumba mbaroni tuhuma kunajisi

**Na Marco Maduhu,**
SHINYANGA

JESHI la Polisi mkoani Shinyanga linawashikilia wanaume wawili akiwamo baba mwenye nyumba kwa tuhuma za kumlawiti mwanafunzi wa kike wa darasa la sita mwenye umri wa miaka 14 (jina limehifadhiwa), mkazi wa Masekelo, Manispaa ya Shinyanga.

Kamanda wa Polisi mkoani Shinyanga, George Kyando akizungumza jana na Nipashe, alisema watuhumiwa hao walikamatwa juzi baada ya kupewa taarifa na mwenyekiti wa serikali ya mtaa juu ya unyama huo.

Alisema baada ya kupata taarifa hiyo, walifika eneo la tukio na kufanikiwa kuwakamata watuhumiwa hao wawili (majina yao yamehifadhiwa ili kuendelea na uchunguzi) na upelelezi ukikamilika watafikishwa mahakamani kwa hatua zaidi za kisheria.

"Jeshi la polisi tunawashikilia wanaume wawili majina yao tumeyahifadhi, mmoja ana umri wa miaka 42 na mwingine 36 kwa tuhuma za kumlawiti mwanafunzi wa darasa la sita mwenye umri wa miaka 14, tukio hili tunalifanyia uchunguzi na tukikamilisha watafikishwa mahakamani," alisema Kyando.

Alisema wanaume hao walikuwa wakimfanyia unyama mtoto huyo kila mmoja kwa wakati wake na vitendo hivyo inaonekana ni vya muda mrefu.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Mtaa wa Luhende katika Kata ya Masekelo, Msafiri Nadula, alisema taarifa za kufanyiwa ukatili mtoto huyo alizipata kutoka kwa baba mwenye nyumba aliyopanga mwanafunzi huyo, ambaye naye kumbe alikuwa akifanya naye vitendo hivyo.

Alisema baada ya kumhoji mtoto huyo, alisema alikuwa akifanyiwa vitendo hivyo na watuhumiwa wote, kila mmoja kwa wakati wake.

"Mtoto huyo ameanza kufanyiwa unyama huu muda mrefu na baba mwenye nyumba ambaye wamepanga, kumbe alinipatia taarifa za mtoto huyu kuwa huwa anarudi usiku saa tano hadi saba, kumbe lengo lake lilikuwa ni kumdhibiti ili asiende kufanya mapenzi na mtu mwingine, bali aendelee kumtumia yeye peke yake," alisema Nadula.

"Baada ya kumbana mtoto huyo kwanini huwa anarudi usiku, ndipo akasema huwa anakwenda kufanya mapenzi kwa mtuhumiwa mmojawapo na kupewa Sh. 2,000, na akirudi nyumbani baba mwenye nyumba naye anamfanyia vitendo hivyo," alidai.




Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF), Dk. John Mduma, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam juzi, kabla ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Prof. Joyce Ndalichako (katikati), kutoa tamko la msamaha wa riba kwa waajiri waliochelewa kuwasilisha michango katika mfuko huo. Kulia ni Mwakilishi wa Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Joseph Nganga. **PICHA: JOHN BADI**

# Serikali yafufua majadiliano mradi Bandari ya Bagamoyo

**Na Gwamaka Alipipi,** DODOMA

SERIKALI imefufua majadiliano na wawekezaji watakaoendeleza Mradi wa Bandari na Kanda Maalum ya Kiuchumi Bagamoyo.

Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Dk. Ashatu Kijaji, alibainisha hayo jana bungeni alipowasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya wizara yake mwaka wa fedha 2022/23, akiliomba Bunge kuidhinisha Sh. bilioni 99.1.

Dk. Kijaji alisema wizara inaratibu uendelezaji wa Mradi wa Bandari na Kanda Maalum ya Kiuchumi Bagamoyo unaolenga kuwezesha nchi kuendana na ushindani wa biashara za usafiri wa majini na muunganisho na shughuli nyingine za kiuchumi ikiwamo viwanda na utalii.

Dk. Kijaji alisema: "Wizara imefufua majadiliano na wawekezaji wa Kampuni za China Merchants Holdings (International) Co. Ltd (CMHI) na Oman Investment Authority (OIA) ambayo awali ilikuwa inaitwa Mfuko wa Uwekezaji wa Serikali ya Oman (State General Reserve Fund - SGRF).

"Majadiliano hayo yanahusu eneo dogo la Mradi wa BSEZ kwa kuendeleza eneo la hekta 3,087 kati ya hekta 9,887, unahusisha ujenzi wa bandari na Kituo cha Usafirishaji (Logistics Park) kwenye eneo la hekta 887 na uendelezaji wa eneo maalum la viwanda (Portside Industrial City) kwenye eneo la hekta 2,200."

Alisema msingi wa marejeo ya majadiliano hayo ambayo yalisimama mwaka 2018 ni kuhakikisha kuwa serikali inatekeleza maeneo ambayo ni wajibu wake kama vile ujenzi wa miundombinu wezeshi (barabara, reli, umeme, maji, gesi na mifumo ya mawasiliano) na lango la kuingilia bandarini kwa maslahi mapana ya Taifa.

Dk. Kijaji alisema uwekezaji katika maeneo ya mradi utafanywa kwa kuvutia wabia wa sekta ya umma na sekta binafsi au kufanywa na mwekezaji binafsi.

Kuhusu vipaumbele vya wizara kwa mwaka wa fedha 2022/23, Dk. Kijaji alivitaja kuwa ni kutekeleza miradi ya kipaumbele iliyoko katika mipango na Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020.

Alitaja kipaumbele kingine ni uwekezaji katika kongani na maendelezo kwenye SEZ, EPZA, kongani za viwanda mfano - kongani ya kigamboni, Kwala na Kitaraka.

Kingine ni usimamizi na udhibiti wa masoko, ushiriki katika shughuli za kikanda -- Jumuiya ya Afrika Masharki (EAC), Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), AfCFTA na kimataifa.

Dk. Kijaji alisema kipaumbele kingine ni kuondoa urasimu katika kuhudumia wawekezaji na wafanyabiashara, kuimarisha ushiriki wa sekta binafsi moja kwa moja katika uchumi na uwezeshaji wa wananchi.

Waziri huyo alitaja vipaumbele mahususi ambavyo ni kuendelea kuratibu programu za uhamasishaji wa uwekezaji ndani na nje ya nchi, kuratibu masuala ya uwezeshaji wananchi kiuchumi na maendeleo ya sekta binafsi.

Kingine ni kuratibu ufanikishaji wa uwekezaji ikiwamo kuongeza ufanisi wa miradi ya uwekezaji kupitia Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC).

Kingine ni kuratibu uanzishaji na uendelezaji wa miradi mikubwa ya uwekezaji yenye manufaa mapana kwa Taifa, kuimarisha mifumo ya kushughulikia kero za uwekezaji.

Alitaja kingine ni kuboresha mazingira wezeshi ya kuendeleza viwanda na biashara kwa kupitia na kutunga sheria, sera na mikakati ya kuvutia uwekezaji.


**KUPOTEA KWA KADI YA GARI**

**ELLEN ANZAMEN SHAYO** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA VITZ** yenye usajili namba **T 468 DNW, CHASSIS NAMBA SCP90202853 na ENGINE NAMBA 2SZ1854306.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

**POLISI TAARIFA: DAR/TAZ/RB/72645/2022**



FORM 58

**IN THE DISTRICT COURT OF TEMEKE**
**AT ONE STOP CENTRE**
**PROBATE AND ADMNISTRATION CAUSE**
**NO. 339 OF 2022**
**In the matter of the state of the late**
**SIMON GABRIEL KITOY**
**and**
**In the matter of application for letters of administration by ESTER JACKSON NITUME**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75)**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceeding if they think fit before the grant of probate (or letters of administration) is made to the above named petitioner
Objections to the grant should be filed on before the **7th day of JUNE, 2022**

**Dated at DAR ES SALAAM this 05th day of MAY, 2022**



**NAFASI ZA KAZI**

Kampuni ya Madawa iliopo Dar es salaam inahitaji **MEDICAL REPRESENTATIVE.**

Kwa mawasiliano piga simu namba **0713 786300.**



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**WILAYA YA MOROGORO**
**LILILOPO MOROGORO**
**NAMBA 64 YA 2021**
**ALSON KIRERI MBWAMBO**
**(Holding power of attorney of**
**YONA LUCAS MAKI ................MUOMBAJI**
**DHIDI YA**
**STAPHEN KEBWE**
**NYABANOSI MARO KYARIGA**
**LEON DYAULI**
**GEOFREY MWAKALINGA**
**PAUL MOSHA ............... WAJIBU MAOMBI**

**WITO/KUITWA SHAURINI**

**KWA**
**STAPHEN KEBWE, NYABANOSI MARO KYARIGA, LEON DYAULI, GEOFREY MWAKALINGA na PAUL MOSHA** popote ulipo Mnaarifiwa ufike katika Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya ya Morogoro tarehe 16/05/2022 mbele ya Mwenyekiti E.MOGOSA wewe mwenyewe binafsi au utume muwakilishi wako bila kukosa ambapo maombi yamepangwa kutajwa.Endapo hautahudhuria maombi yatatajwa na kusikilizwa upande mmoja dhidi yako na kutolewa uamuzi
**Imetolewa kwa MKONO wangu na MUHURI Baraza leo tarehe 28/04/2022.**

**M. KHASIM**
**MWENYEKITI**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W)**
**MOROGORO**

# Waonywa mila potofu sensa

**Na Lilian Lugakingira,** BUKOBA

WANANCHI mkoani Kagera wametakiwa kuweka kando mila potofu kuwa wakihesabiwa watapata madhara badala yake watoe ushirikiano wa kutosha wakati wa sensa ya watu na makazi.

Sambamba na kuelezwa hivyo, wananchi hao wameambiwa kuwa sensa hiyo ina lengo la kuiwezesha serikali kupata takwimu sahihi ambazo zitasaidia kutoa huduma bora.

Akizungumza na Nipashe ofisini kwake kwa ajili ya kujua maandalizi ya sensa hiyo inayotarajiwa kufanyika Agosti, mwaka huu, Mratibu wa Sensa wa Mkoa, Fabian Fundi, alisema hakuna athari zozote zinazoweza kutokea kutokana na mtu kuhesabiwa.

"Tunatumia majukwaa mbalimbali zikiwamo nyumba za ibada na mikusanyiko mingine kuelimisha jamii umuhimu wa sensa. Lakini ninyi vyombo vya habari mtusaidie kuondoa mila potofu zilizoko kwenye jamii kwamba mtu akihesabiwa atapatwa na shida. Hii sensa ni ya sita na kila mwananchi anahesabiwa, je, kuna madhara yoyote yalishawahi kutokea kwa kuhesabiwa?" alihoji.

Alisema kufanyika kwa sensa kunairahisishia serikali kupanga mipango ya namna ya kuwahudumia wananchi wake na kuleta huduma za kijamii kulingana na makundi yatakavyoainishwa wakati wa sensa husika.

Mratibu huyo alisema hata katika familia kila siku lazima kiongozi afahamu kuna idadi ya watu wangapi, ndipo awahudumie kwa usahihi.

Fundi pia aliwataka wananchi kutoruhusu watu wenye ulemavu hasa watoto kufichwa na familia zao ili wasihesabiwe badala yake watoe ushirikiano wa kutosha ambao utawezesha kila mtu kuhesabiwa bila kujali ulemavu alio nao, ili kuirahisishia serikali kuweka mipango thabiti ya kulihudumia kundi hilo.

"Inawezekana mlemavu akafichwa halafu ikaonekana Kagera kuna idadi ndogo ya watu wenye ulemavu. Hii itasababisha wengi kukosa usaidizi. Mfano kuna shule maalumu kwa ajili ya kundi hilo zinajengwa, isipotolewa idadi kamili unaweza kukuta serikali inajenga shule yenye madarasa mawili, kumbe inahitajika yenye madarasa 10," alisema.



Mwenyekiti wa Kamati ya Maadili ya Baraza la Habari Tanzania (MCT), Jaji mstaafu Robert Makaramba, akimwapisha Mhariri Mtendaji wa Gazeti la Nipashe, Beatrice Bandawe, kuwa jaji kwenye tuzo za umahiri wa uandishi wa habari Tanzania (EJAT) 2021, katika hafla iliyofanyika mkoani Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Mchakato wa EJAT 2021 waiva, Samia mgeni rasmi

**Na Halfan Chusi**

KAZI 598 zimewasilishwa kuwania Tuzo ya Umahiri wa Uandishi wa Habari Tanzania (EJAT) Mwaka 2021, huku Rais Samia Suluhu Hassan akitarajiwa kuwa mgeni rasmi katika utoaji wa tuzo hizo jijini Dar es Salaam Mei 28, mwaka huu.

Akitangaza kuanza kwa mchakato wa kuwapata washindi hao, Mwenyekiti wa Kamati ya Maandalizi ya EJAT 2021, Kajubi Mukajanga, aliwaambia waandishi wa habari mkoani Dar es Salaam jana kuwa jumla ya kazi 598 zimewasilishwa kuwania tuzo katika makundi 20, ikiwa ni ongezeko la kazi 202 kutoka kazi 396 zilizowasilishwa kwa ajili ya EJAT 2020.

Mukajanga alibainisha kuwa Rais Samia anatarajiwa kuwa mgeni rasmi katika ugawaji tuzo hizo ikiwa ni mara ya pili kwa Rais aliyeko madarakani kushiriki tukio hilo, Rais wa awamu ya nne, Jakaya Kikwete, alikuwa mgeni rasmi miaka 10 iliyopita.

"Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, ndiye atakayemkabidhi tuzo mshindi wa jumla pamoja na mshindi wa tuzo ya maisha ya mafanikio katika uandishi wa habari.

"Kati ya hizo kazi 598 zilizowasilishwa, waandishi wa Mkoa wa Dar es Salaam wameongoza kwa kuwasilisha kazi 250 wakifuatwa na Mkoa wa Mwanza ambao wamewasilisha kazi 63, Zanzibar kazi 59, Arusha kazi 33 na Tanga kazi 17. Kazi hizo zimewasilishwa na waandishi wa vyombo vya habari 73," alibainisha.

Mukajanga pia alishiriki kuwaapisha majaji saba watakaofanya kazi ya kuchambua kazi zilizowasilishwa ili kumpata mshindi, akibainisha kuwa kuapishwa kwa majaji hao ndiyo kuanza kwa kazi ya kumsaka mshindi.

Aliwataja majaji hao kuwa ni pamoja na mwandishi mzoefu Mkubwa Ally ambaye ataongoza jopo la majaji. Wengine ni: Mwanzo Millinga; Imane Duwe; Rose Haji; Aboubakar Famau; Mbaraka Islam na Mhariri Mtendaji wa Nipashe, Beatrice Bandawe.

Majaji hao waliapishwa na Jaji mstaafu Robert Mkaramba ambaye pia ni Mwenyekiti wa Kamati ya Maadili ya Baraza la Habari Tanzania (MCT) linaloandaa tuzo hizo.

Akizungumza wakati wa kuwaapisha majaji hao, Jaji Makaramba aliwataka kuwa waadilifu na kutenda haki kwa waandishi waliowasilisha kazi zao.

# Aachiwa huru baada ya mtoto kudai hakubakwa

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

MAHAKAMA ya Mkoa Wete imeliondoa shauri la kubaka lililokuwa linamkabili Omar Hemed Abdi (23), mkazi wa Kwale Micheweni, baada ya mtoto wa miaka 12 aliyedaiwa kufanyiwa kitendo hicho kukana.

Akitoa hukumu ya kesi hiyo, Hakimu wa Mahakama hiyo, Omar Ali Abrahman alisema, analiondoa shauri hilo chini ya kifungu cha 103 (a) cha Sheria Na. 7 ya mwaka 2018.

Alisema ameliondoa shauri hilo baada ya mwathiriwa wa tukio hilo kuidhihirishia mahakama kuwa hajawahi kufanyiwa kitendo cha ubakaji na mtuhumiwa huyo, bali alilazimishwa na bibi yake aseme kuwa amebakwa.

"Mahakama hii baada ya kupata ushahidi huo, imeamua kuiondoa kesi iliyokuwa ikimkabili Omar Haed Abdi kutokana na mtoto mwenyewe kudai kuwa hakufanyiwa kitendo hicho na mtuhumiwa," alisema hakimu huyo.

Wakili wa Serikali kutoka Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashitaka Pemba, Juma Mussa Omar, alidai kuwa, kutokana na ushahidi alioutoa mtoto mwenyewe, hakuna sababu ya kuendelea na kesi hiyo kwa kuwa yeye ndie mwenye ushahidi wanaoutegemea zaidi.

"Vitendo hivyo sana hufanyika kwa siri, hivyo shahidi wa kwanza ni mtoto na ndiye ushahidi wake tunaoutegemea zaidi. Lakini ameiambia mahakama kuwa mtuhumiwa huyo hakumfanyia ubakaji bali aliambiwa na bibi yake aseme hivyo," alidai wakili huyo.

Awali ilidaiwa mahakamani hapo Februari 3, 2021 majira ya saa 8:00 usiku katika kijiji cha Kwale Micheweni, Omar Hemed Abdi alimnajisi mtoto wa kike mwenye miaka 12 mkazi wa Kwale Micheweni, jambo ambalo ni kosa kisheria.

Kufanya hivyo, ilidaiwa ni kosa kinyume na kifungu cha 108 (1), (2), (e) na kifungu cha 109 (2), (a) vya Sheria ya Adhabu nambari 6 ya mwaka 2018, Sheria ya Zanzibar.

# Wadau wakuna vichwa matumizi nishati chafu

Na Mary Geofrey

WADAU wa sekta ya Nishati nchini wamejadili kuhusu ripoti ya namna ya Tanzania inaweza kuhama kutoka matumizi ya nishati chafu kuingia kutumia nishati jadilifu.

Ripoti hiyo ambayo ilitolewa kwa kushirikiana na Wizara ya Nishati, inalenga kutoa njia za kufikia upatikanaji wa huduma za nishati nafuu za uhakika, endelevu na za kisasa ifikapo mwaka 2030 nchini.

Ripoti hiyo pia inaonyesha njia za kuongeza usambazaji wa umeme ili kuchochea ukuaji wa uchumi na kuboresha maisha wakati wa kuzuia kufungwa kwa uchafuzi wa mafuta ifikapo 2050.

Akizungumza kwa niaba ya Waziri wa Nishati, January Makamba, Katibu Mkuu wizara hiyo, Felchesmi Mramba, jijini Dar es Salaam jana, alisema lengo ni Tanzania kuhama kutoka nishati isiyo safi ambayo inatumika kwa wingi.

Mkutano huo uliandaliwa na taasisi na kampuni za nchi ya Norway, kuwasilishwa ripoti iliyoandikwa na watafiti kuhusu namna ya kuepuka kutumia nishati chafu zinazoharibu mazingira.

Alisema hali ya matumizi ya nishati jadilifu ni asilimia tano ya umeme ambao uko mkoani Kigoma zinazotokana na jua na mtu mmoja mmoja anayewekeza umeme wa jua kwenye nyumba zao na pampu za maji.

"Sasa hivi nchi hatutumii sana nishati jadilifu ila sasa tupo katika hatua nzuri za kuanza kuwekeza kwa ukubwa zaidi," alisisitiza.

Alisema mkutano huo uliwakutanisha wadau wengi kutoka nchi hiyo na nchi za Ulaya ikiwamo Uingereza wenye lengo la kuwekeza kwenye nishati jadilifu.

Alisema Ubalozi wa Norway umewezesha kufanyika kwa mkutano huo, utakaovutia wawekezaji wakubwa kuwekeza katika sekta ya nishati jadilifu.

Kuhusu ripoti hiyo, alisema imegusia maeneo ya utafiti uliofanyika, kuagalia bei ya kuwezesha kufanikiwa kwa mpango huo, ushiriki wa wazawa na aina ya nishati zinazogusa hadi za kupikia, hususani vijijini.

Akizungumzia ripoti hiyo, Balozi wa Norway nchini, Elisabeth Jacobsen, alisisitiza haja ya dharura ya kuharakisha mabadiliko ya uwezekano wa nishati endelevu.

Meneja Mkuu wa Kampuni ya Uzalishaji Umeme wa Upepo na Maji ya Riftvaley Energy, Degratius Massawe, alisema ripoti hiyo itasaidia uwekezaji katika sekta hiyo. Alisema wanasambaza nishati hiyo kwenye gridi ya taifa kwa zaidi ya Megawati tano na kwamba wanakabiliwa na kero ya msururu wa vibali na havipatikani sehemu moja.

# Mbaroni tuhuma wizi wa vifaa vya zahanati

Na Shaban Njia, KAHAMA

JESHI la Polisi mkoani Shinyanga linawashikilia watu wanane kwa tuhuma ya wizi wa vifaa vya ujenzi wa Zahanati ya Kata ya Ulowa katika Halmashauri ya Ushetu vyenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni tisa vilivyotolewa na wadau wa maendeleo.

Kamanda wa Polisi mkoani humo, George Kyando alithibitisha jana kukamatwa kwa watuhumiwa hao ambao wanadaiwa kuiba vifaa hivyo vilivyotolewa Aprili 30 mwaka huu na Kampuni ya Allience One ili kukamilisha ujenzi wa zahanati hiyo.

Kamanda Kyando alisema kwa sasa wanayahifadhi majina ya watuhumiwa hao mpaka upelelezi utakapokamilika ili wawawafikishe mahakamani.

"Jeshi la Polisi kwa sasa tunaendelea na uchunguzi, tukikamilisha tutawafikisha mahakamani ili kujibu tuhuma zinazowakabili na tunatoa onyo kwa watu wanaoiba vifaa vinavyotolewa kama msaada na wahisani na kujinufaisha kwa manufaa yao binafsi," alisema Kyando.

Awali, akitoa taarifa ya wizi wa vifaa vya ujenzi wa zahanati hiyo, mwenyekiti wa kamati ya ujenzi wa zahanati hiyo, Charles John, alisema baada ya vifaa hivyo kukabidhiwa kwao, alirudi mfanyakazi wa Kampuni ya Allience One kuomba kurudishwa kwa baadhi ya vifaa.

Alisema alilazimika kuwaita wajumbe wa serikali ya kijiji ili kujadili suala hilo ndipo wakaamua baadhi ya vifaa virudishwe ambavyo kwa mujibu wa mfanyakazi huyo vilitolewa kimakosa vikiwamo ndoo tano za rangi pamoja na mifuko ya saruji 43.

Mbunge wa Ushetu, Emmanuel Cherehani, alisema ofisi yake ilipokea taarifa kutoka kwa wananchi juu ya wizi wa vifaa hivyo na kuamua kujulisha vyombo vya dola.

Alisema vifaa vilivyokamatwa katika msako huo ni pamoja na maboksi 75 ya vigae, mikanda 15 ya gypsum, unga wa gypsum, mifuko mitano ya saruji, mali ya Zahanati ya Ulowa ambavyo tayari vilikuwa vimeuzwa kwa mfanyabiashara wa Kata ya Ulowa.

Cherehani aliomba serikali kufanya ukaguzi wa dharura wa na uhakiki vifaa na fedha za miradi yote ya ujenzi wa vituo vya afya na zahanati.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akimkabidhi Meneja wa Benki ya NMB Kanda ya Kaskazini, Dismas Prosper, Tuzo ya Shukrani kwa Benki hiyo kudhamini wiki ya ununuzi wa umma, jijini Arusha juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Majaliwa ataka wanaokaidi ununuzi mfumo kidijitali wachukuliwe hatua

Na Mwandishi Wetu, ARUSHA

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa ameiagiza Wizara ya Fedha na Mipango kuhakikisha taasisi zote za umma zinatumia Mfumo wa Ununuzi kwa Njia ya Mtandao (TANePS) na hatua kali zichukuliwe dhidi ya maofisa masuhuli ambao taasisi zao zitakaidi mfumo huo.

Maagizo hayo aliyatoa jijini Arusha juzi , wakati akifungua kongamano la Wiki ya Ununuzi wa Umma lililowakutanisha wadau wa ununuzi takribani 1,000 wakiwamo maofisa ugavi, wazabuni, wajumbe wa bodi na maofisa masuhuli kutoka wizara, taasisi, halmashauri na sekta binafsi.

Akizungumza katika kongamano hilo, Majaliwa alisisitiza matumizi ya mifumo katika ununuzi wa umma pamoja na kuhakikisha ufanisi wa mifumo hiyo ili huduma zipatikane kwa wakati ukiwemo umakini wa wanaosimamia mifumo na kuwa na njia mbadala ikitokea changamoto ya mtandao.

"Wizara ya Fedha na Mipango ifanye tathmini na maboresho ya mifumo na taratibu za ununuzi ili kudhibiti mianya iliyopo inayosababisha Serikali kupoteza fedha nyingi kwa huduma ambazo kiuhalisia bei zake ni za chini,' alisema Majaliwa.

Alisisitiza kuwa ili kupata thamani halisi ya fedha katika ununuzi wa umma usimamizi madhubuti unahitajika katika sekta hiyo hasa kwa kuzingatia kuwa zaidi ya asilimia 70 ya bajeti ya serikali ambayo inatokana na fedha za walipa kodi, inatumika katika ununuzi wa bidhaa, huduma na kandarasi za ujenzi.

Alisema kipindi kinachoishia Machi, 2022 zabuni 48,487 zenye thamani ya Sh. trilioni 22.7 zimechakatwa, hivyo fedha hizo zinazotumika kwenye ununuzi zinahitaji usimamizi madhubuti kwa kuwa kinahusisha matumizi ya fedha za walipakodi.

Pia Majaliwa aliiagiza Wizara ya Fedha na Mipango kupitia kitengo chake cha Usimamizi wa Mifumo ya Taarifa za Kifedha na GPSA ihakikishe bei zote za bidhaa na huduma zinazotumika sokoni kwa jumla na rejareja zinaingizwa kwenye mfumo wa TANEPS na kuwa na kiwango cha ukomo wa bei zitakazotumika Serikalini.

Aidha, amewataka wadau wa kongamano la Wiki ya ununuzi wa umma kutumia wiki hiyo kuendelea kuhamasishana, kupeana uzoefu na pia kujadiliana namna bora zaidi ya kuendelea kutumia teknolojia kuboresha ununuzi wa umma nchini, pamoja na kuelimisha wananchi umuhimu wa teknolojia katika manunuzi ya umma.

Akizungumza kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Lameck Nchemba, katika kongamano hilo, Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Hamad Hassan Chande, alisema serikali imechukua hatua mbalimbali katika kuboresha sekta ya ununuzi wa umma kwa maslahi ya taifa kwa kufanya maboresho katika Sheria ya ununuzi wa umma.

Alisema maboresho hayo ni pamoja na kurekebisha vifungu vilivyokuwa vinakwamisha utekelezaji wa ununuzi kwa ufanisi na kuhakikisha kuwa sekta ya ununuzi inawashirikisha watanzania wa makundi yote katika kujenga uchumi wa taifa.

"Faida zilizotokana na marekebisho ya sheria ni pamoja na kupungua kwa muda wa mchakato wa ununuzi, ushughulikiaji wa malalamiko ya wazabuni, upendeleo kwa makampuni yanayomilikiwa na watanzania na upendeleo wa makundi maalumu ya vijana, wanawake, wazee na watu wenye ulemavu," alisema Chande.

Alisema serikali imeendelea na jitihada za kuimarisha utekelezaji wa ununuzi wa umma nchini kwa kuanzisha na kusimamia utekelezaji wa mifumo ya kielektroniki katika kudhibiti matumizi na kuongeza ufanisi kwenye ununuzi wa umma.

Pia Chande alisema Wiki ya Ununuzi wa umma inatoa fursa kwa wadau wa ununuzi wa umma na ugavi kubadilishana uzoefu pamoja kufanya maonesho ya huduma wanazotoa kwa jamii.

Kongamano la Wiki ya Ununuzi wa Umma limeandaliwa na Wizara ya Fedha na Mipango na taasisi zinazosimamia ununuzi wa umma nchini ambazo ni Mamlaka ya Kudhibiti Ununuzi wa Umma (PPRA), Wakala wa Huduma za Ununuzi Serikalini (GPSA), Mamlaka ya Rufani za Zabuni za Umma (PPAA) na Bodi ya Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi (PSPTB).

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Isaidieni Serengeti Girls sasa msisubiri mwishoni

**TIMU** ya soka ya Taifa ya wasichana wa umri chini ya miaka 17 (Serengeti Girls), inakabiliwa na mechi ya kusaka tiketi ya kushiriki fainali za Kombe la Dunia (U-17), dhidi ya yosso wenzao wa Cameroon.

Serengeti Girls ni moja kati ya timu sita zilizofika hatua ya mwisho ya kusaka wawakilishi watatu kutoka Afrika watakaofuzu fainali hizo zitakazochezwa baadaye mwaka huu huko nchini India.

Nyota hao wanaofundishwa na Bakari Shime wamefika hatua hiyo baada ya kuwaondoa majirani zao kwenye Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati, Eritrea na Burundi.

Timu nyingine zilizofika hatua ya mwisho ya kusaka tiketi ya kushiriki fainali hizo ni Ethiopia ambayo yenyewe itacheza dhidi ya Nigeria wakati Ghana watapambana na Waarabu wa Morocco.

Nchi tatu zitakazokuwa na matokeo mazuri ndio zitaenda kushiriki fainali za Kombe la Dunia.

Hadi kufikia hatua hii, inaonyesha Serengeti Girls wamepambana vyema kusaka tiketi hiyo, hivyo wanastahili kuungwa mkono ili kufikia malengo na ndoto za Watanzania ambazo zimedumu kwa muda mrefu.

Ili timu ifanye vyema inahitaji misaada mbalimbali ikiwamo vifaa, chakula, malazi bora pamoja na posho ili kuzifanya akili zao ziwaze jambo moja tu la kucheza kandanda.

Nipashe inapenda kulipongeza Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), kwa kuendelea kuihudumia timu hiyo pamoja na timu nyingine za wanawake bila ya kuwapo kwa wadhamini ambao hupunguza makali ya kugharamia mahitaji muhimu ya kila siku.

Tunapenda kuwakumbusha wadau kujitokeza sasa kuwasaidia Serengeti Girls ili kurahisisha maandalizi yao na hatimaye kupata nafasi ambayo wanaililia kwa muda mrefu ya kushiriki fainali za Kombe la Dunia kwa mara ya kwanza. Kumbukeni kampuni na taasisi zinapowekeza kuanzia kwenye maandalizi, hapo ndio inakuwa imefanya uamuzi sahihi na kuacha ile tabia ya kusubiri timu ikate tiketi na kuanza kuipatia fedha hali ya kuwa wakati wa maandalizi haikupata misaada stahiki.

Wachezaji wanapopata maandalizi sahihi sasa, yatasaidia kufuzu lakini pia yatawafanya waende katika fainali hizo (endapo wataifunga Cameroon), wakiwa imara kila idara na si kusindikiza mataifa mengine.

Mpira wa miguu wa wanawake umebadilika na huu ni muda sahihi kwa wadau wa michezo nchini kuliangalia soka hilo kwa jicho makini na kuacha tabia ya kusubiri kumwagilia maji matunda yaliyochanua bila kushiriki wakati wa kuyapanda.

Tunaamini hadi hatua ambayo mmefikia, Serengeti Girls pamoja na benchi la ufundi mnafahamu heshima ambayo mtaiweka endapo mtafanikiwa kuifunga Cameroon katika mechi ya kwanza ugenini na ile ya marudiano itakayochezwa hapa nchini (kwenye Uwanja utakaotangazwa hapo baadaye).


Pamoja na kulitangaza vizuri jina la Tanzania kupitia soka hilo la wanawake, tunawakumbusha wachezaji kufahamu mechi hizo zinaweza kubadilisha maisha yao kwa kuonekana na mawakala na makocha wa klabu mbalimbali za nje ikiwamo Ulaya na hatimaye kusajiliwa kwa dau nono. Ni wazi kwenye soka hakuna miujiza, timu iliyojiandaa vizuri na yenye wachezaji wanaotekeleza vyema majukumu yao kulingana na nafasi zao uwanjani ndio itakayosonga mbele, hivyo tuungane pamoja kuhakikisha timu hii inapata maandalizi bora na ambayo yataiweka Tanzania kwenye ramani na rekodi mpya duniani.

Hakuna jambo lisilowezekana, kama mwaka huu tumefanikiwa kufika hatua ya mwisho ambayo haijawahi kufikiwa na timu ya wanaume (Taifa Stars), basi inawezekana kupitia Serengeti Girls, ikafungua njia ya mafanikio kwa timu za Tanzania.

Kwenye nia Mungu hufanya wepesi, mbali na wadhamini, mashabiki wa soka jiandaeni kujitokeza kwa wingi kuishangilia timu hii pale itakaporejea nyumbani na kuwakaribisha wapinzani wao Cameroon katika mechi hiyo ya marudiano.

Serengeti Girls inawahitaji Watanzania na Watanzania wanahitaji timu hiyo. Isaidieni ili itimize ndoto zake. Mungu ibariki Serengeti Girls, Mungu ibariki Tanzania.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Adam Fungamwango

## Muungwana Lazima Nilonge

# Kama timu zinashangilia kutoka sare, ligi ni dhaifu

**NILIWAHI** kuandika huko nyuma kuwa nina mashaka na kile kinachosemwa Ligi Kuu ya Tanzania Bara ni bora.

Nikaandika inawezekana ikawa ni kweli, lakini kwangu mimi ambaye nimeshawahi kuiona Ligi ya Tanzania miaka ya 1980 hadi 1990, bado ilinipa mashaka kuamini moja kwa moja kitu hicho.

Nikizikumbuka zile timu za wakati ule zilivyokuwa zikileta ushindani kwenye ligi, nikaona hizi za siku hizi ni dhaifu. Tena dhaifu sana.

Wakati nikiendelea kuwa na mashaka hayo, Meneja Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally ameibuka na kusema kile kile nilichokibainisha kwamba Ligi Kuu Tanzania Bara ina timu dhaifu.

Inawezekana ikawa alichelewa kufanya uchunguzi wake, lakini angalau amekwenda ambako mimi nilikuwa nafikiria. Akaandika kwenye mtandao wake wa kijamii wa instagram maneno yafuatayo.

"Katika timu 16, timu 14 zinaweza kushuka daraja, hii sio aina ya ligi tunayoihitaji, haiwezekani timu nyingi zigombanie kushindwa. Ligi yenye ushindani ni ile ambayo timu nyingi zinagombania ubingwa, timu nyingi msimu huu zimekua dhaifu, tupo raundi ya 22 lakini ni timu tatu tu zimefikisha pointi angalau 30. Msimu uliopita hadi kufika raundi ya 22, timu saba zilikua na pointi angalau 30.

Hii ni hatari kwa sababu bingwa anaweza kupatikana kwa kufunga wadhaifu wengi.

Najua utauliza kwanini na wewe usiwafunge hao dhaifu wengi ili uwe bingwa? Ukweli ni kwamba katika hizo mechi zetu dhidi ya timu dhaifu nasi tulifanya udhaifu." Aliandika Ahmed.

Kiungo wa zamani wa Waziri Mkuu, Simba na Tiimu ya Taifa (Taifa Stars), Mtemi Ramadhani naye akaungana na Meneja Habari huyo wa Wekundu wa Msimbazi kusema ligi ni dhaifu kwa sababu kuna timu dhaifu.

"Wakati mwingine unaangalia mpira unashangaa, huyu kweli ndiyo mchezaji ambaye juzi alitoka kucheza mechi dhidi ya Simba au Yanga? Ni kwamba timu zingine zinakuwa na mechi mbili au tatu kwa msimu, zikicheza na Simba, Yanga, au wakati mwingine Azam, lakini zikicheza zenyewe, huoni kama kweli wanapambana. Kinachonisikitisha hata wakicheza na Simba au Yanga wanakamia badala ya kucheza soka, na wakipata bao, badala ya kucheza soka wanaanza kupoteza muda, kipa anavua glovu, wachezaji wanafanya vituko ambavyo nia yake ni kupoteza muda tu, haiwezi kuwa ligi ya ushindani," alisema Mtemi.

Ally Mayay, mchezaji wa zamani wa CDA, Yanga na Taifa Stars naye alikiri kuna matatizo, lakini akasema kutokana na udhamini ambao kwa sasa umeanza kuingia kwenye soka unaweza kuanza kupungua. Wanaosema haya ni wachezaji waliocheza miaka ya nyuma, wanajua wanachokizungumza, kwa sababu hata mimi nimewaona kwa macho yangu wakicheza soka.

Binafsi ninavyojua hata miaka ya nyuma, Simba na Yanga zimekuwa zikipokezana ubingwa wa Tanzania Bara na Muungano, ingawa ulikuwa unaingiliwa na timu nyingine katikati kama Coastal Union, Pamba, Tukuyu Stars, Prisons, Mseto, Comsmopolitan, Pan African, lakini kulikuwa na ushindani mkubwa tofauti na sasa.

Ukiangalia kwa sasa Simba na Yanga zinachukua ubingwa kirahisi zaidi. Zamani wakati mwingine zililazimika kusubiri hadi mechi za mwisho ndiyo ziamue.

Ukitaka kujua timu kwenye Ligi Kuu ni dhaifu, angalia zikicheza na Simba au Yanga, zinakaa nyuma, zinahitaji zaidi sare kuliko ushindi, zikibahatika kupata bao moja, basi ni hilo hilo. Tena wataanza kupoteza muda kama alivyobainisha Mtemi.

Ndiyo maana zikipata sare , wachezaji wao wanashangilia na kuzunguka uwanja, unaweza kudhani zimetwaa ubingwa. Timu inayosaka ubingwa haiwezi kushangilia sare dhidi ya Simba au Yanga. Jiulize Simba au Yanga, kufungwa mabao 2-0, 3-0, 3-1, ilikuwa lini?

Miaka ya nyuma, Simba au Yanga kupigwa idadi hiyo ya mabao ilikuwa ni kitu cha kawaida tu, tena ikiwa na wachezaji bora kabisa wanaochezea mpaka Taifa Stars.

Mfano mdogo ninaokumbuka haraka haraka, Simba iliwahi kuchapwa mabao 4-2 na Reli ya Morogoro, Uwanja wa Jamhuri, siku hiyo hiyo Yanga ikabamizwa mabao 3-0 dhidi ya Pamba, Uwanja wa Taifa. Zinafungwa na hazikamiwi, ila zinachezewa mpira haswa.

Hakuna kupaki basi. Na haikuwa mara ya kwanza mbili au tatu kufungwa na timu mbalimbali kwa idadi kubwa ya mabao. Hii ndiyo unaweza kusema ligi bora na timu zilikuwa bora. Kwa hizi timu zinazoshangilia sare, zikicheza kutaka kusalia Ligi Kuu, naungana na wote wanaosema ligi ya Bongo ni dhaifu kwa sababu ina timu dhaifu.

## Mradi wa maji miji 28 waiva

WAZIRI wa Maji, Jumaa Aweso, amesema taratibu zote zinazohusu miradi ya maji kwenye miji 28 itakayotekelezwa kwa fedha za mkopo kutoka serikali ya India kupitia Benki ya Exim zimekamilika.

Pia amesema kabla ya makadirio ya mapato na matumizi ya wizara hiyo, watakutana na wabunge ili kukubaliana lini mradi utiwe saini kwa kuwa taratibu zote tayari.

Aweso aliyasema hayo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la nyongeza la Mbunge wa Geita (CCM), Joseph Musukuma.

Mbunge huyo alisema mradi wa miji 28 ni mkombozi kwenye majimbo ambayo hawajawahi kukutana na maji ya bomba.


"Mheshimiwa Waziri kila nikiuliza mnasema mwezi mmoja. Unaniambia nini ili wananchi wangu wapate faraja ya miradi ya miji 28?" alihoji

Akijibu swali hilo, Waziri Aweso alisema taratibu zote zimekamilika na sasa kinachosubiriwa ni kutia saini ili mradi uanze kutekelezwa.

Awali, Katika swali la msingi, Mbunge wa Geita Mjini (CCM), Costantine Kanyasu, alihoji ni lini serikali itajenga upya bwawa la Kasamwa pamoja na kutenganisha miundombinu ya kunyweshea mifugo ili kuondoa muingiliano wa binadamu na mifugo.

Akijibu swali hilo, Waziri Aweso alisema bwawa hilo lilijengwa kwa ajili ya shughuli mbalimbali za kijamii ikiwamo kutoa huduma za maji kwa ajili ya matumizi ya binadamu, viwanda, kunyweshea mifugo pamoja na kilimo.

"Katika mwaka wa fedha 2022/23, serikali itafanya usanifu kwa ajili ya kukarabati bwawa hilo. Kazi hii pia itajumuisha miundombinu kwa ajili ya kunyweshea mifugo," alisema.




**Habari zote na Augusta Njoji,** DODOMA

# Wabunge walia uhaba wataalamu

SERIKALI imeshauriwa kuajiri wataalamu wa saikolojia wengi zaidi ili kukabiliana na ongezeko la matukio ya ya mauaji nchini ambayo yanatokana na watu kuathirika kisaikolojia.

Rai hiyo ilitolewa jana na wabunge katika kipindi cha maswali na majibu bungeni.

Mbunge wa Viti Maalum, Esta Maleko, katika swali lake alihoji kama serikali haioni umuhimu wa kuongeza wataalam wa saikolojia kwenye jamii ili kutoa huduma za ushauri wa afya ya akili na namna ya kuondokana na msongo.

"Pamoja na kwamba serikali kupitia vyuo vikuu inatoa mafunzo ya saikolojia, kwa nini isiajiri watalaamu wa saikolojia ili kupunguza tatizo la mauaji kila kukicha? Pia kwanini isiwe na mpango wa kusajili chama cha watalaamu wa saikolojia kama zilivyo taaluma zingine?" alihoji.

Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Fatma Toufiq, alihoji serikali haioni imefikia wakati wa kuanzisha kliniki tembezi kutoa huduma hiyo ya saikolojia sehemu mbalimbali.

Kwa upande wake, Mbunge Viti Maalum (CCM), Shally Raymond, alisema tatizo la saikolojia kwa sasa ni kubwa kiasi cha wananchi wengi kuishia kwenye hospitali za watu wenye matatizo ya akili ikiwamo Mirembe kutokana na kukosa tiba ya kisaikolojia.

Kutokana na hali hiyo, alihoji serikali lini itaona umuhimu wa kutoa mafunzo hadharani wakati wakishughulikia suala la ajira za watalaamu wa saikolojia.

Akijibu maswali hayo, Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi, Mwanaidi Ali Khamis, alisema kuna tatizo la uhaba wa watalaamu wa saikolojia nchini.

Hata hivyo, alisema serikali inaendelea kushirikiana na Ofisi ya Rais, Tawala za Miko ana Serikali za Mitaa (TAMISEMI) ili kupata kibali kuajiri watalaamu hao kadri bajeti itavyoruhusu.

Pia alisema suala la kuunda bodi ya wataalamu hao wa saikolojia, serikali ipo kwenye mchakato wa kuunda bodi ya wataaamu wa ustawi wa jamii itakapokamilika itawasajili watalaamu hao.

Alisema serikali inatambua umuhimu wa wanasaikolojia hao, inajipanga ili kuhakikisha pale inapopata nafasi za ajira inawaajiri.

"Suala la kuanzisha kliniki zinazotembea za tiba ya kisaikolojia wapo watalaamu hawa kila Mikoa na wanafanya kazi katika Halmashauri hadi vijijini," alisema.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akisalimiana na Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Mendeleo ya Makazi, Ridhiwani Kikwete kwenye viwanja vya Bunge, jijini Dodoma, jaan. Mbunge wa Viti Maalum, Felister Njau. **PICHA: OWM**

# Uundaji bodi za parole mikoa wakamilika

SERIKALI imekamilisha kuunda bodi za msamaha kwa wafungwa (Parole) katika mikoa yote nchini, ili kutimiza wajibu wa bodi hizo za kukaa vikao na kupunguza tatizo la msongamano wa wafungwa, imeelezwa.

Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Jumanne Sagini, aliyasema hayo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la nyongeza la Mbunge wa Mafinga Mjini (CCM), Cosato Chumi.

Chumi katika swali hilo alitaka kujua kwa nini bodi hizo zimesaidia kutoa msamaha kwa wafungwa 70 tu wakati wako zaidi ya wafungwa 15,000 waliohitaji kupitiwa na kusamehewa.

Alisema inawezekama iko mikoa ambayo bodi hiyo vikao vyake havifanyiki na kuhoji serikali ina mpango gani kusaidia katika hilo kama sheria inavyoelekeza.

Akijibu maswali hayo, Naibu Waziri Sagini alisema kutokana na bodi nyingi kumaliza muda wake mwaka 2020/21, wafungwa waliopata msamaha kupitia Bodi ya Parole nchini ni 70.

Hata hivyo, alikiri kuwa sheria ya kuanzisha bodi hizo za Parole iliwekwa ili kusaidia kupungumza msongamano magerezani.

"Sheria iliwekwa ili bodi isaidie kupunguza msongamano gerezai nikiri mwaka 2021 vikao havikukaa kwa sababu bodi nyingi ziliisha muda wake lakini tayari bodi zimeshaundwa," alisema.

Katika swali la msingi, Chumi alihoji bodi za mkoa na kitaifa zinafanya vikao mara ngapi kwa mwaka na wafungwa wangapi wamepata msamaha kupitia bodi hizo kwa mwaka 2020/21.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Sagini alisema Bodi ya Parole ya Taifa na Mikoa ziliundwa kwa Sheria namba 25 ya mwaka 1994 na ikafanyiwa marekebisho na Sheria namba 5 ya Mwaka 2002 kwa lengo la kutaka wafungwa wengi wanufaike na mpango huo.

Alisema bodi hizo kisheria zinatakiwa kufanya vikao vyake angalau mara nne kwa mwaka.




Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko (kulia), akimkabidhi Mkuu wa Polisi wa wilaya hiyo, John Kafumu, viti, meza na stuli kwa ajili ya matumizi ya Kituo kipya cha Polisi katika Mgodi wa Madini ya dhahabu Mwakitolyo, wilayani humo, jana. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Waziri ataka teknolojia ya kisasa udhibiti upotevu mazao ya samaki

**Na Mbaraka Kambona,** KIGOMA

NAIBU Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, amewataka wadau wa uvuvi kutumia teknolojia ya kisasa ili kudhibiti upotevu wa mazao ya samaki, hususan dagaa.

Amesema sekta hiyo inakabiliwa na matatizo mbalimbali ikiwamo upotevu wa dagaa, hivyo kuikosesha serikali mapato na kwamba kwa kutumia teknolojia hiyo, ana matumaini kero hiyo itaondoka.

Ulega aliyasema hayo juzi mkoani hapa alipokuwa akizindua maadhimisho ya miaka 10 ya Mradi wa Tuungane unaotekelezwa na mashirika ya kimataifa ya Tanzania Nature Conservancy na PathFinder International kwenye vijiji vya kusini mwa mwambao wa Ziwa Tanganyika.

Alisema ni muhimu kufahamu kwamba upotevu wa mazao ya uvuvi katika ukanda wa Ziwa Tanganyika ni mkubwa , hivyo wadau wa maendeleo ukiwamo mradi wa Tuungane, kuwekeza zaidi kwenye teknolojia ya ukaushaji wa dagaa na kuwaepusha wavuvi na hasara.

"Kama kweli tunataka kuwawezesha wavuvi wetu basi tuwekeze katika ukaushaji wa dagaa. Jambo hili ni muhimu sana kwa mustakabali wa watu wetu," alisema.

"Tusiruhusu kuona dagaa ambao wanaweza kuwainua Watanzania wa chini kuendelea kupoteza matumaini kutokana na upotevu wa mazao yao hasa katika kipindi cha mvua," alisisitiza

Waziri Ulega aliupongeza mradi wa Tuungane kwa kuwajengea vichanja vya kuanikia dagaa wavuvi wanaofanya shughuli zao katika ukanda wa Ziwa Tanganyika na kuongeza kuwa kitendo hicho kinaunga mkono nia ya Rais wa Samia Suluhu Hassan ya kukuza uchumi wa bluu nchini.

Pia aliwapongeza kwa kuimarisha vikundi vya ulinzi shirikishi wa rasilimali za uvuvi katika mwambao wa Ziwa Tanganyika ambao umewezesha kuongezeka kwa rasilimali za uvuvi kwenye ziwa hilo hasa kutokana na ulinzi na uhifadhi wa maeneo ya mazalia ya samaki na dagaa. Hata hivyo, alisema haitoshi kuishia kuhifadhi maeneo ya mazalio ya uvuvi na kuongeza uzalishaji bali kuna haja sasa ya kuwa na teknolojia za kisasa zitakazowawezesha wavuvi kuchakata mazao yao na kuyaongezea thamani.

Awali, Mkurugenzi Mkuu wa Tanzania Nature Consevancy (TNC), Lucy Magembe, alisema katika kipindi cha miaka 10 kupitia mradi wa Tuungane, wamehifadhi maeneo ya mazali ya samaki na maeneo ya uvuvi yenye ukubwa wa hekta 12,015 katika wilaya za Uvinza mkoa Kigoma, Mlele na Tanganyika wilaya ya Katavi.

Mkuu wa Wilaya ya Uvinza, Hanaf Msabaha, alisema licha ya serikali kufanya kazi kubwa katika kutekeleza miradi mbalimbali ya uvuvi kwenye mwambao wa Ziwa Tanganyika, utekelezaji wa mradi wa Tuungane umewezesha kupunguza uvuvi haramu, kutoa elimu kwa wavuvi na wachakataji wa mazao ya uvuvi ambao wamewezesha kwa sasa dagaa wa Kigoma kuwa na thamani kubwa na kuwa na soko kubwa nje ya nchi.

## Wadau wa tiba asili waiangukia serikali

**Na Romana Mallya**

WADAU wa tiba asili wamemwomba Rais Samia Suluhu Hassan kuwaangalia kwa ukaribu na kuwajengea mazingira wezeshi katika kazi zao, hasa kwenye utafiti.

Mvumbuzi na Mwasisi wa Dawa ya 4A9, Dk. Twalibu Msigwa, alitoa rai hiyo jana mkoani Dar es Salaam alipozungumza na waandishi wa habari, akisimulia kuwa amekuwa miongoni mwa wanaowasilisha utafiti Wizara ya Afya kwa lengo la kuwa na mbadala wa kutumia aina nyingine za dawa.

"Nimekuwa nikikusanya maoni kwenye bonde ambalo ninalifanyia utafiti na kuyapeleka Wizara ya Afya na nakala zake kwa Rais, nimefanya hivyo kwa vipindi vinne," alisema.

Mdau huyo wa tiba asili alisema alidai kuwa kuwapo binti alikwenda ofisini kwake akilia kutokana na kusumbuliwa na moja ya magonjwa makubwa na alifanikisha matibabu yake.

Dk. Msigwa pia aliiomba serikali aiangalie uwezekano wa kupunguza bei pindi wanaposajili dawa zao kwa kuwa tiba ya asili inao uwezo wa kutatua magonjwa sugu nchini.

# Wanataaluma maendeleo ya jamii wapewa elimu

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

WATAALAM wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, wametakiwa kuifanya taaluma hiyo kuwa kamili na inayotambulika kisheria.

Rai hiyo ilitolewa jana na Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maaalum, Dk. Dorothy Gwajima, wakati akizungumza na wataalam wa maendeleo ya jamii waliowakilishwa na baadhi ya wajumbe wa Chama cha Wataalam wa Maendeleo ya Jamii (CODEPATA).

Dk. Gwajima alisema uwapo wa Sheria ya Kuundwa kwa Taaluma ya Maendeleo ya Jamii itasaidia taaluma hiyo kuwa na nguvu kwenye utekelezaji wa majukumu yao katika mikoa na halmashauri.

Alisema changamoto wanazopitia watalaam wa maendeleo ya jamii, ikiwamo ya watu wasio wanataaluma kupangiwa majukumu ya maendeleo ya jamii, hivyo uwapo wa sheria itasaidia kutatua changamoto hizo.

"Taaluma ya maendeleo ya jamii lazima iwe kwa mujibu sheria ikawa na bodi na bamalka yake itasaidia kutatua changamoto nyingi zianawakabili wataalam hawa na jamii yetu pia," alisema Dk. Gwajima.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Zainab Chaula, alisema wataalam wa maendeleo ya jamii wanapaswa kuwa chachu ya maendeleo na mabadiliko ya fikrsa na kusaidia jamii kutatua changamoto zinazowakabili kwa kuwapa ufumbuzi na namna ya kukabiliana nazo.

"Ukipita katika mitaa huko tunaona watu wengi wanapambana maisha hasa wanawake hao ndio wetu. Tuwasaidie kutatua changamoto zao ili wajikwamie kiuchumi," alisema Dk. Chaula.

Rais wa CODEPATA, Angela Mvaa, alimshukuru Dk. Gwajima kwa nasaha na maelekezo yake na kwamba chama hicho kitahakikisha kinaweka nguvu ya kuwa na sheria ambayo itabadilisha mtazamo na mwelekeo wa taaluma ya maendeleo ya jamii nchini.





# Wajasiriamali watonywa fursa kuhusu filamu ya Royal Tour

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

BAADA ya Rais Samia Suluhu Hassan kufanya uzinduzi wa Filamu ya Royal Tour kwa mara ya kwanza nchini, wajasirimali mkoani Dodoma wametakiwa kuanza kuchangamkia fursa ambazo zinatarajiwa kujitokeza kupitia tukio hilo.

Katibu wa Wajasiriamali mkoa wa Dodoma, Christopher Dioniz, alibainisha hayo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu fursa zinazoweza kujitokeza mara baada ya uzinduzi wa filamu hiyo.

Alisema tukio hilo ambalo lilifanyika jijini Arusha likiongozwa na Rais Samia, linatoa fursa nyingi kwa wajasiriamali ambazo wanaweza kuzitumia ili kujikwamua kiuchumi na kukuza mitaji ya biashara zao.

"Filamu hii ambayo Rais Samia Suluhu Hassan ameizindua hivi karibuni jijini Arusha, itafungua fursa nyingi kwetu, hivyo ni wajibu wa kila mmoja wetu kuhakikisha anafanya kitu ambacho kitakuwa na tija kwake na taifa kwa ujumla,"alisema Dioniz.

Alisema kila mjasiriamali anapaswa kuwa mbunifu katika kile anacho kifanya ili wakati wa fursa kufunguka kupitia filamu hiyo utakapofika anufaike.

"Wajasiriamali lazima tuwe wabunifu katika shughuli zetu za kila siku ikiwa ni pamoja na kutumia TEHAMA (Teknolojia ya Habari na Mawasiliano) kujitangaza ili kunufaika na fursa ambazo zitakazojitokeza kupitia filamu hiyo ya kutangaza utalii iliyoandaliwa na Rais Samia," alisema.

Kadhalika, aliomba serikali kutenga maeneo yatakayotumiwa na wajasiriamali kuendesha shughuli zao pamoja na kupatiwa mafunzo kupitia Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO).

"Pia ili kufanikisha shughuli za ujasiriamali ni lazima halmashauri kutoa fedha za mikopo za asilimia 10 kwa wakati kwa vikundi pamoja na kufuatilia maendeleo ya miradi ya vikundi mbalimbali ili kuwe na tija badala ya kuvitelekeza," alisema Dioniz.

Meneja Mwendeshaji wa Hoteli ya GerWill ya jijini hapa, Miraji Kapaso, alisema kutokana na Dodoma kukua kwa kasi, kuna haja ya wawekezaji kuwekeza katika sekta mbalimbali zitakazowezesha wageni kupata huduma.

"Zamani ilikuwa akija balozi lazima atafute ndege ya kumrudisha Dar es Saalam kutokana na kukosekana na sehemu nzuri za hoteli. Lakini hivi sasa ziko sehemu nyingi ambazo zinaweza kuwahudumia wageni watakaokuja kwa ajili ya shughuli za kibiashara na kitalii,"alisema.




Rais wa Chama cha Wakunga Tanzania (TAMA), Feddy Mwanga, akizungumza katika maadhimisho ya Siku ya Wakunga Duniani kitaifa, jijini Dodoma juzi iliyohudhuriwa na wadau mbalimbali likiwamo Shirika la Umoja wa Mataifa la Masuala ya Afya ya Uzazi na Idadi ya Watu (UNFPA) Tanzania. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Naibu Waziri ageukia madereva malipo faini

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

NAIBU Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Jumanne Sagini, amewataka wamiliki na watumiaji wa vyombo vya moto kuzingatia na kufuata sheria za usalama barabarani ikiwamo kulipa madeni wanayodaiwa bila kushurutishwa.

Sagini aliyasema hayo jijini Dodoma jana wakati akizindua mashine mpya za kisasa za POS kwa ajili ya kukusanyia maduhuli ya Jeshi la Polisi hususani kikosi cha usalama barabarani.

Pamoja na kutumika katika ununuzi wa silaha, hati ya tabia njema na kukusanyia tozo mbalimbali hasa kwa madereva wasiofuata sheria za usalama barabarani.

Aidha, alisema mashine hizo mpya zinatumia mfumo wa Android yenye 'wireless' na uwezo wa kuskani leseni, kuchukua alama za vidole na kupiga picha jambo ambalo litasaidia kupunguza malalamiko ya wananchi yaliyokuwapo.

Sagini alilipongeza Jeshi la Polisi nchini kwa kutumia wataalamu wake wa ndani kuendeleza mfumo huo ambao alisema utapunguza malalamiko na kuwawezesha kutekeleza majukumu yao bila kutumia nguvu kubwa.

"Kwa sababu mfumo huu kwa sasa unachukua taarifa muhimu kwa dereva, hivyo hawezi kuja kukataa kwa sababu alama za vidole vyake havifanani na mtu mwingine dunia nzima. "Nawapongeza sana naamini mfumo huu utakwenda kuwa chanya kwenu na kwa wananchi. Hatutegemei kupata malalamiko tena ya kuwapo kwa makosa katika kumwandikia mtu kosa," alisema Sagini.

Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini, Inspekta Jenerali (IGP) Simon Sirro, aliwataka watumiaji wa barabara, hususani madareva, kutii sheria bila shuruti na kutoa ushirikiano pale askari wa usalama barabarani wanapotaka kuchukua taarifa zao kwa ajili ya kujiridhisha wanapoandika au kufanya ukaguzi wa vyombo vya moto.

"Kwa mashine hizi mpya inahitaji dereva achukuliwe alama za vidole, picha na kuskani leseni. Sasa niwaombe usiwe mbishi pale askari anapotaka taarifa hizi mtoe ushirikiano. Kikubwa tii sheria bila kushurutishwa,"alisema IGP Sirro.

Mkuu wa kitengo cha TEHAMA wa Jeshi la Polisi, Kamishna Msaidizi (ACP) Dawson Msongaleli, alisema mfumo huo ulianza kwa kufanyiwa majaribia kwa mikoa ya Dar es Salaam na Pwani mwaka 2017 na baada ya kufanya kazi vizuri ndipo mwaka 2018 wakaanza kutumia kwa mikoa yote ya Tanzania Bara.

Alisema nia ya kutumia mashine hizo ni kuondokana na mlundikano wa watu katika vituo vya polisi na kusababisha foleni isiyokuwa na ulazima.

# Gwajima aibua mambo yaliyojiri mikutano jinsia

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, ametoa mrejesho wa mikutano miwili ya kimataifa aliyoshiriki.

Mikutano hiyo ni ule wa 66 wa Kamisheni ya Umoja wa Mataifa kuhusu Hali za Wanawake Duniani uliofanyika nchini Marekani na wa G7 Care Work uliofanyika nchini Ujerumani.

Dk. Gwajima akizungumza na wadau mbalimbali wa masuala ya wanawake na jinsia jijini Dodoma jana, alisema Tanzania ilishiriki mikutano hiyo kwa lengo la kwenda kujifunza na kueleza duniani nini Tanzania inafanya katika kuwawezesha wanawake kiuchumi na usawa wa kijinsia.

"Mimi binafsi nilialikwa na nilishiriki katika mkutano huo ambapo niliambatana na mtaalamu mmoja. Mkutano huo ni muhimu sana kwa kuwa kama mnavyofahamu Mama Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, aliahidi kuwa kinara wa utekelezaji wa eneo la pili kuhusu Haki na Usawa wa Kiuchumi kwenye Jukwaa la Usawa wa Jinsia," alisema Dk. Gwajima

Alisema lengo la mikutano hiyo muhimu ni kujadili masuala mbalimbali ya maendeleo ya wanawake ikiwamo mafanikio na changamoto zilizopo zipate uamuzi wa kisera na kiutekelezaji kutoka kwa viongozi na wataalam.

"Nimeitisha kikao hiki ili nitoe mrejesho wa mikutano hiyo miwili na pia kuweka mikakati ya utekelezaji wa maazimio ya mikutano hiyo na kupitia kikao hiki pia nitaomba tujipange vizuri zaidi ili kuwa na ushiriki bora zaidi katika mikutano hii kwa wakati mwingine" alisisitiza.

Dk. Gwajima aliwashukuru wadau waliowezesha ushiriki wa Tanzania katika mkutano wa 66 wa Kamisheni ya Umoja wa Mataifa kuhusu hali za Wanawake Duniani na ule wa Mkutano wa G7 Care Work ambao ni UN Women, UNFPA, Ubalozi wa Ireland na Asasi ya LSF, LANDESA na OXFAM ambazo zilichangia katika kuwezesha Viongozi na wataalam kushiriki mikutano hiyo.

"Ninaomba nitoe rai kwa wadau wengine wa Maendeleo kuendeleza ushirikiano huu na kutuwezesha kwa utaalam na rasilimali fedha na kushirikiana nasi katika maeneo mbalimbali kadri tutakavyoendelea kuwasiliana nao na kuwashirikisha kwenye maeneo yetu ya vipaumbele." alisema Dk. Gwajima

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka, alisema mkoa wake uko tayari kushirikiana na wizara na wadau wengine kuhakikisha suala la kuwawezesha wanawake kiuchumi na usawa wa kijinsia ili kuwezesha kufikia azma ya Rais Samia.





Muuguzi Mkuu wa Halmashauri ya Mji Masasi, mkoani Mtwara, Devotha Namahala (kulia), akitoa ufafanuzi wa matumizi ya kifaa tiba na mashine ya oksijeni kwa Meneja wa Vodacom Tanzania Foundation, Sandra Oswald, alipotembelea Hospitali ya Mkomaindo mjini Masasi mapema wiki hii, ili kujionea utendaji kazi wa vifaa vilivyotolewa na taasisi hiyo kwa ajili ya kusaidia matibabu ya watoto njiti hospitalini hapo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# SMZ yasisitiza faida ukodishaji visiwa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imesema ukodishwaji wa visiwa vidogo vya Unguja na Pemba umelenga kuleta tija na kuinua sekta ya Utalii.

Pia imesema hatua ya ukodishwaji huo ilitokana na baadhi ya visiwa hivyo kutumika vibaya kwa ajili ya kusafirisha dawa za kulevya.

Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Lela Muhamed Mussa, alisema hayo jana wakati akifafanua hoja zilizoibuliwa na wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kuhusu ukodishwaji wa visiwa vidogo vilivyoko Unguja na Pemba katika kikao cha baraza.

Baadhi ya wajumbe walichangia makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Rais Kazi na Uwezeshaji Kiuchumi, walionyesha kutoridhishwa na ukodishwaji wa visiwa hivyo na kudai wananchi hawajashirikishwa kikamilifu.

Lela ambaye alikuwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale, alisema uwekezaji katika visiwa vidogo ni muhimu na umelenga kuongeza pato la taifa.

Alisema kwa muda mrefu visiwa vidogo vimekaa bila ya kutumiwa kwa ajili ya shughuli muhimu za kuingiza fedha na uwekezaji katika sekta ya utalii.

Alibainisha kuwa ukodishwaji wa visiwa hivyo utaimarisha utalii ambao unaweza kugawanywa katika sekta mbalimbali ikiwamo utamaduni na utalii wa kuzamia baharini.

Lela alisema mchakato wa kukodisha visiwa hivyo ulianza tangu mwaka 2009 na ilipofika mwaka 2019 serikali iliunda kamati maalumu chini ya watu 17 kufanya tathmini kuhusu mchakato huo.

"Mheshimiwa Spika, niwajulishe wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwamba suala la ukodishwaji wa visiwa vidogo vidogo pamoja na matumizi yake, serikali ya awamu ya nane haijakurupuka tu na kufanya uamuzi huo. Mwaka 2019 iliundwa kamati ya watu 17 wakiwamo wataalamu wa sekta mbalimbali pamoja na mazingira na ardhi na Kikosi Maalumu cha Kuzuia Magendo (KMKM)," alisema.

Lela pia alisema baadhi ya visiwa vidogo vilivyoko Unguja na Pemba, vilikuwa vikitumiwa vibaya katika usafirishaji na uingizaji wa dawa za kulevya.

Alisema maharamia waliokuwa wakijishughulisha na biashara ya dawa za kulevya walikuwa wakitumia nafasi hiyo na baadhi ya visiwa vilikuwa jirani na baadhi ya nchi hasa Kenya katika eneo la Mombasa.

Waziri alisema kwa muda mrefu baadhi ya visiwa vidogo vilikuwa vikitumika kwa wananchi kufanya ziara za kitalii bila ya serikali kupata mapato.

Alibainisha kuwa baadhi ya nchi zilizopiga hatua kubwa katika sekta ya utalii duniani wamevitumia visiwa vidogo vidogo na kuvikodisha kwa wawekezaji mbalimbali ili kuingiza fedha.

Alisema nchi kama Maldives na Shelisheli ambazo ni visiwa na zina visiwa vidogo vidogo vingi, zilivikodisha kwa wawekezaji hatua ambayo imeziingizia fedha nyingi na utalii wao kuwa maarufu duniani kote.

# Mwinyi kuzindua filamu Royal Tour leo

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, leo anatarajiwa kuzindua filamu ya Royal Tour kwa upande wa Zanzibar, hafla itakayofanyika katika hoteli ya Golden Tulip mjini hapa.

Akizungumza jana na waandishi wa habari, Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari, Sanaa, na Utamaduni, Dk. Hassan Abbasi, alisema filamu hiyo itaitangaza Tanzania kupata wawekezaji wengi katika sekta mbalimbali.

Dk. Abbasi alisema filamu hiyo imeshaanza kupata matokeo mazuri na kuna programu kubwa katika sekta ya sanaa na utamaduni.

Alisema filamu hiyo itaisaidia Tanzania kuunganishwa na mataifa mbalimbali ili kuwa na wawekezaji wengi katika sekta ya utalii.

Kwa mujibu wa Katibu Mkuu huyo, gharama iliyotumika katika filamu hiyo imesharudi na kwamba imegharamiwa na sekta mbalimbali za binafsi.

"Gharama iliyotumika katika filamu hii tayari imesharudi na chenji imebaki, hivyo tunaweza kuandaa programu nyingine," alisema.

Alisema kwa namna ya viongozi wa kitaifa walivyojitoa kutangaza makala hiyo ni lazima kuwapongeza kwa jitihada zao hizo.

Pia alisema filamu hiyo itaoneshwa katika vituo vyote vya televisheni Tanzania kuanzia kesho baada ya kufanyika uzinduzi huo kitaifa jijini Dar es Salaam.

"Tunahaki ya kuisambaza filamu yetu hii katika vituo vyetu vya televisheni Tanzania bure kwa sababu tuna hakimiliki hiyo," alisema.

Filamu hiyo, alisema itauzwa katika televisheni 350 nchini Marekani na matarajio yao ni kutazamwa na watu bilioni moja duniani.

Alisema lengo la filamu hiyo ni kufikisha faida kubwa kwa kuitangaza nchi duniani, kupata watalii,viwanda na maendeleo kwa ujumla.

# Wawekezaji wazawa wapatiwa kipaumbele

**Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imesema itaendelea kuhamasisha wawekezaji wazalendo kuwekeza na kwamba wamepewa kipaumbele cha kwanza kutumia fursa hiyo muhimu kukuza uchumi na pato la taifa.

Hayo yalisemwa jana katika kikao cha Baraza la Wawakilishi na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Kazi na Uwekezaji Kiuchumi, Mudrik Ramadhan Soraga, wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Kwahani, Yahya Abdalla Rashid.

Mwakilishi huyo alitaka kujua faida za uwekezaji kwa wananchi wazalendo nchini na wanapewa nafasi gani katika kushiriki maendeleo ya uchumi kupitia uwekezaji.

Alisema mwenyeji anayetaka kuwekeza katika sekta ya utalii anapaswa kuwa na kima cha mtaji usiopungua Dola za Kimarekani 300,000 wakati mgeni atalazimika kisheria awe na mtaji usiopunguwa Dola milioni 2.5.


Pia alisema fursa zingine zimetajwa na Mamlaka ya Uwekezaji Vitegauchumi Zanzibar (ZIPA) ambazo zinapatikana kwa wenyeji tu ikiwamo kuongoza kampuni za kutembeza watalii nchini au kumiliki.

Alisema kwa nyakati tofauti, ZIPA imefanya mikutano mbalimbali na wawekezaji pamoja na wafanyabiashara kutangaza fursa za uwekezaji zinazopatikana nchini katika sekta hiyo.

Waziri Soraga aliwataka wananchi wazalendo na wafanyabiashara kujitokeza kuchangamkia fursa hizo za uwekezaji ili kuchangia pato la taifa katika sekta hiyo yenye ukuaji mkubwa.

Alisema katika uwekezaji wa viwanda mbalimbali, serikali imeweka mkazo kwa wananchi wazalendo kujitokeza kuwekeza kwani fursa ziko nyingi.

"Kwa upande wa uwekezaji katika viwanda, ziko fursa nyingi kwa wafanyabiashara wazalendo wenye nia ya kuwekeza.



**ODEMBA**
UKURASA 12



Nipashe
MWANGA WA JAMII
BT



# KAJIENGUA WCB?

## Rayvanny afuta taarifa zote muhimu

UTATA unazidi kuikumba lebo ya muziki ya WCB, kutokana na hatua ya mmoja wa wanamuziki wake, Rayvanny, kuonyesha ishara kwamba hayupo tena katika familia hiyo.

Rayvanny ambaye hivi sasa anamiliki kampuni yake inayoitwa Next level Music, ameondoa taarifa muhimu pamoja na picha zinazoihusu WCB ambayo inamilikiwa na Diamond Platnumz.

Mwanamuziki huyo, katika maelezo muhimu yanayomuhusu, anaelezea yeye ni Ofisa Mtendaji wa NLM na pia ni mshindi wa tuzo za BET pekee.

Maelezo kama yeye ni moja ya wanamuziki wa WCB ambayo huko nyuma yalikuwepo, ameyaondoa na hakuna picha yoyote ya lebo hiyo ambayo ameposti au kushiriki.

Muda mrefu kumekuwepo na uvumi kwamba Rayvanny anaondoka WCB na kwenda kutafuta changamoto nyingine kama alivyofanya Harmonize, lakini mwenyewe alikana na kueleza bado yupo sana.

Kuondolewa kwa taarifa hizo katika ukurasa wa Rayvanny ambao unafuatiliwa na mamilioni ya watu, ni ishara kwamba sasa hayupo tena na anafanya kazi binafsi.

Hata hivyo Rayvanny hakutaka kusema chochote kuhusu hatua yake ya kufuta taarifa hizo.

Mmoja wa viongozi wa WCB, Mkubwa Fela alikaririwa akisema kuna mmoja wa wasanii yupo njiani kuondoka na hajafanyiwa mambo machafu kama wanavyodai wengine.

BASI SAWA

## Maskini Mwijaku kapatikana



MSANII wa filamu za Bongo Muvi, Burton Mwembe, maarufu kama Mwijaku, amekutwa na kesi ya kujibu katika shtaka la kusambaza picha za utupu kinyume na sheria.

Hakimu wa Mahakama ya Hakimu Mkazi, Kisutu,Rhoda Ngimilanga ametangaza uamuzi huo baada ya upande wa Jamhuri kufunga ushahidi wa mashahidi watano na vielelezo vinne.

Mwijaku anadaiwa kutenda kosa hilo kati ya Septemba 17, 2019 na Oktoba 2019 katika jiji la Dar es Salaam. Anadaiwa kuchapisha picha za ngono kupitia mtandao wa kijamii wa WhatsApp uliounganishwa katika kompyuta.

## Steve bado unayo hadi leo?

MCHEKESHAJI Steve Nyerere, amesema haoni uchungu kuondolewa katika nafasi ya usemaji katika shirikisho la muziki kwa kuwa chokochoko zilitokana na kundi la wahuni wachache.

Steve amesema kupingwa kwake ni jambo la kawaida katika maisha na kwamba kuna baadhi ya watoto wanawapinga baba zao wazazi, hivyo kwake sio la kushangaza.

"Waliondesha kampeni ile ninawafahamu ni kundi la wahuni wachache wanaofanya vurugu zao, lakini natambua kuwa anayekuua ni ndugu yako," amesema.





## Odemba hapati usingizi kwa Ibraah

Gumzo limetawala katika mitandao ya kijamii, baada ya mwanamitindo maarufu Miriam Odemba, kuonekana kufa na penzi tamu analopata kwa mwanamuziki kutoka Konde Gang, Ibraah.

Odemba katika ukurasa wake wa Instagram, kila siku hakosi kumsifia Ibraah, kiasi ambacho watu wameacha kufuatilia mambo mengine na badala yake wanamtupia jicho mrembo huyo kila wakati kujua nini atakisema.

Moja ya machapisho yake ya hivi karibuni ameandika "Nimegundua watu wanafurahi sana mimi nikiwa singo, kumtaja tu bebi boi wangu kelele lundo. Mimi na mpenzi wangu wa maisha tunawakaribisha,"



## Harmonize kajipaka doa mwenyewe

MWANAMUZIKI wa Bongo Fleva. Harmonize, amesema hawezi kumpiga mtu ndani ya kituo cha polisi kwa sababu anaheshimu sheria za kila nchi.

Hivi karibuni mwimbaji huyo alikuwa na kashfa akiwa nchini Kenya baada ya kulalamikiwa na mchekeshaji Eric Omondi, kuwa alimpiga ngumi mdomoni wakati akidai pesa ambazo walimpatia kwa ajili ya kufanya onyesho.

"Siwezi kumpiga mtu mbele ya polisi,Eric ni ndugu yangu, mimi nimekuwa nikumuona na kumkubali kila akija Tanzania, namchukulia kama kaka yangu siwezi kufanya jambo hilo," amesema.

## Mzimu wa Yakobo: Kiboko ya utajiri wa mchongo

**Na Adam Fungamwango**

"HIVI mume wangu siri hii ikijulikana dunia itatuchukuliaje?" "Punguza mawazo mke wangu, hili suala mimi nitalimaliza."

"Mume wangu dunia hadaa, ulimwengu shujaa." "Mke wangu acha wasiwasi nani atajua?"

Ni majibizano kati ya Salim na mkewe kwenye filamu ya 'Mzimu wa Yakobo.'

Siku chache baadaye, familia hiyo inampokea mgeni. Ni dada wa Salim. Baada ya masaa kadhaa anamuulizia ndugu yake Yakobo. Mke anamwambia kuna sehemu ametumwa kwenda na kaka yake na atarejea siku chache zijazo.

Nandy, dada yake Salim anamuuliza pia kaka yake juu ya ndugu yao Yakobo. Anajibiwa jibu tofauti na lile la wifi yake. Majibu haya tofauti yanamchanganya.

Anatumwa sokoni na wifi yake, Nandy anakutana na msichana ambaye ni jirani ya kaka yake Salim walipokuwa wakikaa zamani, na wanafahamiana kwa sababu huwa mara kwa mara anawatembelea akitoka kijijini.

Rayuu, anampa pole Nandy kuhusu kifo cha kaka yake Yakobo. Nandy anachanganyikiwa. Rayuu anamwambia Yakobo alifariki ghafla baada ya kuumwa kichwa.

Nandy anarejea nyumbani na kumuuliza kuhusu suala hilo, akilalamika kwa nini kaka yake Yakobo amefariki lakini wameficha bila ya kuleta taarifa kijijini?

Mke wa kaka yake anamtuliza kwa kumwambia asimsikilize Rayuu ni mbea, Yakobo yupo hai na atamuona.

Hata hivyo bado Nandy ana wasiwasi na utajiri wa ghafla wa kaka yake, kwani kwa sasa wanaishi kifahari, tofauti na zamani alipokuwa akiwatembelea kutoka kijijini, wakiishi kwenye mazingira ya ufukara jirani na akina Rayuu.

Usiku wa manane, Salim anamuamsha dada yake na kumwambia anakwenda kumuonyesha utajiri wa dhahabu na madini mengine alipoyafukia ili hata akifa yeye achukue huo utajiri na hataki mkewe ajue.



Wakati wako vichakani, mzimu wa Yakobo unatokea kati yao. Wanashtuka. Mzimu unajitambulisha kwa Nandy yeye ndiye Yakobo na aliuawa na kaka yake Salim na tamaa ya utajiri, na ndiyo siri ya utajiri alionao. Mzimu unasema hata yeye Nandy kupelekwa hapo ilikuwa auawe kwa sababu anaonekana kuanza kujua siri hiyo. Mzimu wa Yakobo unamwambia Nandy kuwa yeye ndiye atarithi huo utajiri, na hatomuacha hai kaka yao Salim kwa alichokifanya.



## TRUMPET, KWENYE VIGODORO, KUSUTANA

**Na Adam Fungamwango**

KWENYE miaka ya karibuni imekuwa si rahisi kuona muziki wa dansi umehanikizwa na chombo cha muziki kiitwacho 'trumpet' kwa kiswahili tarumbeta.

Bendi karibia zote za muziki wa dansi za zamani kuanzia miaka ya '50 hadi mwishoni mwa '90 zilikuwa ni lazima ziwe na ala za upepo ikiwemo trumpet, tena zikipigwa na watu kuanzia watatu hadi watano wakati mwingine.

Mwanzoni mwa mwaka 2000, yalipokuja mapinduzi na muziki kwa ujio wa bendi za African Stars 'Twanga Pepeta', Diamond Sound, FM Academia na nyinginezo, ziliacha kutumia ala za upepo kama trumpet, saxaphone na vingine vinavyofanana na hivyo na badala yake kutumia zaidi kinanda.

Kwa sasa utamu wa chombo hicho umebakia kwenye muziki wa vigodoro ambapo ala za upepo ikiwemo trumpet hupigwa huko na kuwapagawisha akinamama vilivyo kwenye sherehe mbalimbali za kijamii, harusi, kutunzana, na mengine yanayofanana na hayo, ikiwemo hata kwenda kusutana.

Wafuatao ni baadhi ya wapiga trumpet hodari kwenye muziki wa dansi Tanzania, wengine wakiwa hai na baadhi wamefariki.

**Roman Mng'ande 'Romario'**

Huyu ndiye mpiga trumpet maarufu sana kwenye kizazi cha sasa. Na amekuwa maarufu zaidi si kwa sababu ya kupiga trumpet tu, bali hasa machachari yake kwenye kurap, na kucheza hasa akiwa tumbo wazi, huku akikatika.

Ni mwanamuziki wa muda mrefu kwenye kundi la Msondo Ngoma Music.

**Machaku Salum**

Alikuwa mpiga trumpet maarufu kwenye bendi ya Sikinde. Umaarufu wake ulitokana na upigaji chombo hicho pamoja na utanashati wake anapokuwa jukwaani.

Machaku ambaye ameshafariki dunia, ndiye baba mzazi wa aliyekuwa mchezaji wa zamani wa Simba, Salum Machaku.

**Hamisi Mnyupe**

Ni mpiga trumpet mahiri nchini ambaye kwa sasa anapiga bendi ya Msondo Ngoma Music.

Hata hivyo, kabla ya bendi hiyo alishawahi kupitia kwenye bendi za Uda Jazz na Vijana Jazz na hadi leo analisongesha gurudumu la muziki wa dansi nchini akiwa anapiga chombo hicho.

**Joseph Lusungu**

Kiongozi, mtunzi, mpanga muziki, mwalimu na mpiga trumpet wa kiwango cha hali ya juu aliyewahi kuishi nchini.

Ana uwezo wa kuachiwa kipande na kupiga peke yake kwa dakika hata tano, akiwa na uwezo pia wa kupiga kwa staili ya macharanga na muziki wa Cuba na Amerika ya Kusini. Alikuwa ni mmoja wa viongozi wa bendi ya Msondo Ngoma hadi alipofariki.

**Mawazo Hunja Shaurimbele**

Kijana mmoja mtanashati, mwenye uwezo wa hali ya juu kwenye upigaji wa chombo hicho.

Hadi anafariki, alikuwa anapiga bendi ya Vijana Jazz, akiwa amechukuliwa kutoka Super Matimila.





# Ray J usilie uliyataka mwenyewe

MWANAMUZIKI wa Marekani Ray J, amemlalamikia Kim Kardashian na mama yake Kris Jenner, kuwa walishirikiana kusambaza kanda yao ya ngono.

Ray J, ambaye alikuwa na uhusiano wa kimapenzi na Kim, amesema hayo wakati akihojiwa na Daily Mail, amesema yeye hafahamu chochote kuhusu kuvuja kwa video hiyo.

"Sijawahi kuvujisha chochote. Sijawahi kuvujisha kanda ya ngono maishani mwangu. Haijawahi kuvuja. Imekuwa ni makubaliano na ushirikiano kati yangu na Kris Jenner na Kim, na tumekuwa washirika tangu wakati huo, mwanzo wa jambo hili," alisema.

Ray J alisema Kardashian alimpa mama yake mkanda huo na kisha kuwauzia Vivid Entertainment, yeye na Kardashian walisaini mkataba wa kuruhusu video tatu.



## Edochie wake wenza ni shida

MWIGIZAJI wa filamu kutoka Nollywood, Yul Edochie, amesababisha vurugu mtandaoni baada ya mkewe wa kwanza May, kuandika maneno yenye hasira.

Hivi karibuni Edochie,alitangaza kuwasili kwa mwanawe na mke wake wa pili, Judy Moghalu kupitia ukurasa wake wa Instagram.

Hata hivyo, May alijibu kwa hasira kupitia akaunti yake ya Instagram, maneno makali yanayoashiria kuchukia.

"Mungu na awahukumu nyote wawili," ameandika May.

Katika chapisho la Edochie liloambatana na picha, aliandika "Ni wakati wa dunia kukutana na mwanangu. Anaitwa Star Dike Munachimso Yul Edochie, amezaliwa na mke wangu wa pili ninampenda sana, kama vile ninavyowapenda watoto wangu wengine,"

## Prince Kid hali bado tete

HALI bado tete kwa mwandaaji wa mashindano ya urembo nchini Rwanda na mwanamuziki mashuhuri wa zamani, Dieudonne, ambaye amekamatwa kwa tuhuma za unyanyasaji wa kingono.

Dieudonne Ishimwe kwa jina la umaarufu Prince Kid, alitiwa mbaroni na polisi kwa tuhuma za uhalifu unaohusiana na unyanyasaji wa kingono, kulingana na idara ya upelelezi ya Rwanda.

Imeelezwa utaratibu unafanyika kesi hiyo kufikishwa kwa mwendesha mashtaka kwa muda unaofaa kulingana na sheria.





## Nkechi kweli hutaki kurudi nyuma

MSANII wa filamu wa kike kutoka Nigeria, Nkechi Blessing Sunday, amewapa ushauri wafuasi wake wa mtandaoni wa kutorudi nyuma wakati wanapotafuta mapenzi.

Nkeshi alifumwa hivi karibuni akiwa na rafiki yake ambaye anadaiwa kuwa ana uhusiano wa kimapenzi na Opeyemi Falegan.

"Bila kujali ni nini kinashuka katikati ya machafuko usisahau mapenzi ni kitu kizuri.Nina upendo mwingi ndani yangu na kwamba siogopi kupenda. Kuna wakati unajipenda zaidi, inakuwa rahisi kupenda na kupendwa, usikate tamaa juu ya mapenzi,." Ameandika.

## Chappelle ashambuliwa jukwaani

MSANII wa ucheshi kutoka Marekani Dave Chappelle, amepata tukio la kushtushwa baada ya kuvamiwa na mtu mmoja mwenye kisu wakati yupo jukwaani akiburudisha.

Kulingana na taarifa mbalimbali, tukio hilo lilitokea katika ukumbi maarufu wa Hollywood Bowl, mbele ya watu waliokuwa wakihudhuria tamasha lake.

Mshambuliaji huyo huyo alikuwa na kisu chenye umbo la bunduki, lakini alikamatwa.

Katika video ambayo imesambaa mitandaoni inaonyesha mtu huyo akimuangusha chini Chappelle na alijaribu kukimbia nje ya jukwaa kabla hajakamatwa na wana usalama.



# Taarifa ya hali ya hewa inavyochagiza ustawi wa wakulima, wafugaji vijijini

Na Faustine Feliciane



Kilimo kinakuwa na tija endapo taarifa muhimu za hali ya hewa zinapatika kwa wakati

KATIKA msimu huu wa mvua kwa mikoa ambayo inapata mvua mara mbili kwa mwaka, imeonyesha kutarajia kupata neema, hivyo wakulima wanatakiwa kutumia vizuri kwa ajili ya kilimo.

Awali msimu uliopita mikoa hiyo ikiwemo nyanda za kaskazini mikoa ya Manyara, Arusha, Kilimanjaro na Tanga, ilikumbana na hali ya kuwa na mvua chache zilizosababisha ukame kwa baadhi ya maeneo hayo.

Mkoa wa Manyara ni miongoni mwa maeneo yaliyokumbana na ukame mkubwa uliopelekea hasara kwa wakulima, wafugaji na wananchi wengine kwenye maeneo yao.

Katika Wilaya ya Kiteto, ambao ni kinara kwa ufugaji na kilimo cha mahindi ndani ya mkoa huo, zaidi ya mifugo 25,000 ilikufa kutokana na ukame msimu uliopita.

Mkuu wa Wilaya hiyo, Mrakibu Mwandamizi wa Uhamiaji Mbaraka Batenga, anasema ukame uliacha majonzi kwa jamii ya wafugaji na wakulima tofauti.

Akizungumza na gazeti hili katika ofisi za Halmashauri ya Wilaya hiyo, Batenga, anasema mwaka jana uzalishaji wa chakula na mazao ya mifugo ulishuka kwa kasi na kutishia ustawi wa jamii.

"Mbali na mazao kunyauka na maeneo mengine kutoota kabisa, mifugo zaidi ya 25,000 kwa ujumla wake ilikufa kwa kukosa maji na malisho," anasema Batenga.

Anaongeza "Wakulima hawakupata kitu kutokana na mazao kutoota na kustawi vizuri na maeneo mengine hayakuota kabisa na kuleta tishio la njaa ingawa hatukufikia huko, hii yote ni kutokana na ukame,"

Mkuu huyo wa Wilaya anaeleza kufuatia changamoto walizozipitia, aliitisha kikao cha kamati ya maafa kujadili nini cha kufanya ili kukabiliana na hali hiyo kwa siku za usoni.

Anasema kamati hiyo iliamua kuanzisha utaratibu wa kusambaza taarifa za hali ya hewa kutoka Mamlaka ya hali ya hewa Tanzania (TMA) kwa wakulima na wafugaji kwa njia ya simu na kwenye mikutano ya kijamii.

"Kuanzia ngazi ya wilaya mpaka vijijini tunazifuatilia kwa karibu taarifa zote za TMA, ule utabiri wao wa siku wiki mpaka mwezi pamoja na ule wa msimu mzima. Lengo ni kujaribu kujitahadharisha kwa hali yoyote mbaya ambayo tunaweza kukutana nazo kwenye kila msimu," anasema Batenga.

Akifafanua zaidi, anaeleza wameanzisha makundi ya mtandao wa simu ya 'Whatsapp' kwa baadhi ya wakulima, wafugaji, watendaji na wenyeviti wa vijiji wenye simu janja ambao nao wanasaidia kuwapatia wengine wasio na simu hizo taarifa muhimu za hali ya hewa.

Mkuu huyo wa wilaya anasema wamejidhatiti hajiepusha na vifo vingine vya wanyama kwa sababu ya ukame kama ilivyotokea msimu uliopita. Anasema kwa kufuata taarifa za hali ya hewa na ushauri wa TMA, kwa msimu huu walijipanga kikamilifu kukabiliana na hali yoyote mbaya itakayotokea.

Akizungumzia njia walizozitumia msimu huu kuepukana na madhara waliyoyapata msimu uliopita, Ofisa Wanyamapori wa Wilaya hiyo (DGO) Dorice Gama, anasema vifo vya wanyama pori na mifugo vilitokana na hali ya kugombania maji yaliyokuwa kwenye mabwawa na visima vichache vya asili kati ya mifugo, wanyama pori na binadamu.

"Hii kwetu imekuwa kama funzo, kwa sasa kuna visima na mabwawa ambayo yamechimbwa na yamejaa maji ya mvua iliyonyesha, hii itasaidia kuwa na uhakika wa maji kwa muda mrefu," anasema Dorice.

Aidha, anaeleza baada ya kupata utabiri wa mvua msimu huu, walichukua hatua ya kuchimba na kupanua mabwawa ili kuvuna maji ya mvua.

"Kwenye kata ya Makame ambapo kuna makazi ya watu ambao wanaishi ndani ya maeneo ya hifadhi ya wanyama tumechimba bwawa kubwa na kujengea kingo za kuvuna maji, " anasema Dorice

Kwa upande wake mmoja wa wakulima katika kijiji cha Napalai kilichopo kata ya Makame, Joseph Ibrahimu anasema ukame uliwaathiri lakini kwa sasa wamejipanga kukabiliana na hali hiyo.

"Mifugo ilikufa, binafsi zaidi ya wanyama 18 walipoteza maisha, lakini kwa kushirikiana na halmashauri sasa tumekuwa tukifuatilia taarifa za hali ya hewa kwa kutumia magrupu yetu kwenye simu janja na mikutano ya mara kwa mara ya wanavijiji na viongozi wetu, anasema Ibrahimu.

Pia anaongeza kwamba uwepo wa maji na malisho ya kutosha kwa wanyama wao na wanyamapori kumewapa uhakika wa maisha yasiyo na mashaka.

"Msimu uliopita tulikuwa tunagombania maji ya visima na wanyama pori na mifugo yetu, lakini kwa sababu mabwawa yamejaa wanyama wanapata maji na sisi tutatumia kwa uhuru," anasisitiza.

Kufuatia juhudi na tahadhari zinazochukuliwa na Wilaya hiyo ya Kiteto, Meneja wa Kituo Kikuu cha Utabiri cha Mamlaka ya Hali ya Hewa (TMA), Samwel Mbuya, anasema jambo la kuigwa kwa maeneo mengine kuwa na matumizi sahihi ya utabiri wa hali ya hewa.

Anasema ukame ambao ulitokea kwenye baadhi ya mikoa msimu uliopita, hasa Manyara umewapa ukumbusho wa kufuatilia taarifa za TMA.

"TMA tunaendelea kuhimiza matumizi sahihi ya taarifa zetu, walichofanya Wilaya ya Kiteto na wananchi wake ni jambo la kuigwa na kuiunga mkono Serikali katika kuhimiza matumizi sahihi ya taarifa za hali ya hewa kwa maendeleo yao," anaeleza Mbuya.

Anasema TMA itaendelea kufuatilia mifumo ya hali ya hewa na kutoa taarifa sahihi kwa wananchi ili kuzitumia kwenye mipango ya kimaendeleo wanayoipanga.



Mifugo inaweza kuathiriwa na ukame kama hatua muhimu ya kukabiliana na hali hiyo haitachukuliwa.

TULIKOTOKA, TULIPO & TUNAPOKWENDA...



# Visa, vituko, mikasa, madenti wa zamani

## ■Shuleni pekupeku, vifuu, bagia visheti
## ■Kutwangana siku ya kufunga shule

Na Adam Fungamwango

BAADA ya kutoka makala ya safu hii Jumamosi iliyopita, yenye kichwa cha habari 'Nyimbo za Mchakamchaka shuleni enzi hizo' zilimiminika meseji na simu nyingi mno zikionyesha kuguswa vilivyo.

Waliokuwa wakipiga simu na kutuma meseji hizo wengi wao ni wale ambao walisoma enzi hizo na kushiriki kuimba nyimbo mbalimbali zikiwemo zile za kuwananga Nduli Idd Amin Dada, Oscar Kambona na Rais wa zamani wa Malawi, Kamuzu Banda. Sababu nilizielezea.

Wengi walipongeza na kuongeza nyimbo zingine ambazo hazikuwekwa kwenye makala hiyo.

Kikubwa kuliko yote ni kwamba pamoja na nyimbo hizo, wengi walikumbuka maisha ya shule zamani jinsi yalivyokuwa.

Wakatuma meseji kuelezea juu ya mikasa, visa na vituko ambavyo walivifanya, kuvipitia, au kutokea enzi hizo wakati wengine wanasoma shule ya msingi, wengine sekondari na mpaka vyuoni.

Waliotuma meseji wengi wao ni wale waliokuwa wanafunzi miaka ya 1980 kurudi nyuma. Kila mmoja alielezea jinsi maisha yake shuleni yalivyokuwa, alivyokuwa akiishi na wenzake, tabia za walimu, wao wenyewe na mikasa mbalimbali.

Wapo waliokumbushia jinsi enzi hizo asilimia 80 mpaka 90 kama siyo 98 ya wanafunzi walikuwa wakienda shule pekupeku.

Ni kweli kabisa. Kwa vijana wa sasa wanaweza kuona kama ni uongo, au ni kama hadithi za kusadikika, lakini kwa wakati huo ilikuwa ni jambo la kawaida kabisa. Ilikuwa ni ajabu zaidi kumuona mwanafunzi amevaa viatu kuliko akiwa pekupeku.

Yupo kijana yeyote wa sasa anaweza kuona kama wazazi wakati huo walikuwa wazembe, hawawajali watoto wao, au hawakuwa na mapenzi na watoto wao. Pia wala hawakuwa masikini kihivyo.

Ni kwamba enzi hizo za ujamaa maisha ya watu wengi yalifanana. Hakuna mtu aliyekuwa tajiri sana, wala masikini sana. Nadhani wazazi waliona kulikuwa na mahitaji mengine zaidi ya muhimu kwa mtoto wake kuliko kumnunulia viatu, ikizingatiwa karibuni wote walikuwa wanakwenda hivyo hivyo.

Pia hata kama mtoto alikuwa na viatu, hivyo vilikuwa vya kuendea safari na si shule. Zamani kulikuwa na nguo za sikukuu, za kushindia nyumbani maarufu kama 'nguo za kubugia', na za kwenda kutembelea ndugu.

Kuna waliojaribu kwenda na viatu, lakini wakiona wenzao wanatembea pekupeku, nao wanaona hakuna haja ya kwenda navyo.

Wengine walikwenda na kandambili, ambazo kwa sasa maarufu kama ndala. Hizi hizi ambazo mtoto wa sasa hawezi kabisa kwenda nazo shule, wanafunzi walikwenda nazo na kuonekana nyumbani kwao mambo safi.

Enzi hizo ni kwamba siku ya Ijumaa, wanafunzi walitakiwa kwenda na vifuu vya nazi kwa wale waliosoma maeneo ya Dar es Salaam na Pwani.

Wale wa mikoani na vijijini ilikuwa ni kwenda na jembe, vidumu vya maji, maua, mbolea, fagio na pia hata kupeleka kuni shuleni. Hakukuwa na mabegi kama sasa. Badala yake ilitengenezwa mifuko ya karatasi, na hasa mabaki ya mifuko ya saruji, ikitengenezwa na gundi la uji wa muhogo, mifuko yake ilitumika sana kuwekea madaftari.

Madenti wengine waliamua tu kuchukua madaftari kama mawili, kukunja na kuweka kwenye mfuko wa nyuma wa kaptura ya shule. Kulikuwa na wanafunzi watemi, hasa wale waliokuwa wakipenda kukaa kwenye madawati ya nyuma. Ni kama ilikuwa fasheni hivi. Kwanza walikuwa watemi, pili wana umri mkubwa, halafu wengi wao hawakuwa makini sana darasani. Na hii ilikuwa hivyo hivyo karibuni shule zote. Waliitwa wazee wa 'backbencher'.



**MADENTI WENYEWE WAFUNGUKA**

Baada ya hayo, hebu tuangalie simu na meseji za madenti wa zamani walivyotiririka kuelezea maisha ya shule enzi hizo. Wengi hawakutaka majina yao yachapishwe hapa kwa sababu mbalimbali.

Baadhi yao ni watu wenye nyadhifa sehemu mbalimbali nchini.

"Mwanzoni mwa miaka ya 80, nakumbuka darasa letu aliyekuwa akivaa viatu alikuwa mmoja tu. Hiyo ilikuwa mkoani Kimanjaro.

Asilimia 98 ya wanafunzi wa shule yetu tulikuwa hatuvai viatu. Hii ilikuwa ni shule ya msingi." Huyu ni mwanafunzi wa shule moja mkoani Kilimajaro.

"Nakumbuka shuleni kwetu hakukuwa na mwanafunzi aliyekuwa akivaa viatu, ikafikia kipindi walimu wakasema kama baba yako hajakununulia viatu vaa vya kwake, kwani tunawaona kwenye vilabu vya pombe wamevaa viatu kwanini washindwe kuwanunulia na nyie?" Ilikuwa ni meseji na mdau mmoja walivyokuwa wakinangwa na walimu.

"Nakumbuka nasoma shule ya sekondari, waliokuwa wanavaa viatu walikuwa hawazidi watano." Ni meseji wa aliyekuwa denti wa sekondari wakati huo.

"Kuna shule ya msingi niliwahi kusoma kwa muda kijijini alikokuwa akiishi bibi yangu. Huko wanafunzi walikuwa wanakuja wamejifunga migolole. Yaani unakuta mwanafunzi ana nguo moja tu, hiyo hiyo shule, na nyumbani pia, Hakuna sare." Ni mdau aliyekuwa akisoma kijijini.

"Mimi na dada yangu tulikwenda kwenye shule moja kijijini tukiwa na sare na viatu. Dada yangu akapewa cheo cha Dada Mkuu, kwa kuwa alikuwa kwenye madarasa ya juu kuliko mimi." Mdau mwingine denti wa zamani huyo alitupasha.

"Hahaha, mimi nakumbuka walikuja watoto kutoka mjini, walikuwa na sare safi na viatu vizuri mno. Hawakuwa vizuri darasani hasa masomo ya sayansi na hesabu. Nilikuwa darasa la tatu, nikawa nawafundisha, kwao walikuwa na uwezo, asubuhi nikawa naletewa maandazi na vihela nilikuwa napata kidogo." Huyu alielezea jinsi akili yake ilivyomsaidia kukabiliana kidogo na njaa shuleni.

"Mimi nakumbuka nikiwa darasa la tano, mwalimu mmoja wa sayansi, akija darasani lazima aje na fimbo kama kumi hivi, anaanza kukumbushia somo la mwisho, anayeshindwa anapita mbele, anapigwa fimbo sita, aisee kweli nimekumbuka mbali sana."

"Kuwahi namba saa moja pia ilikuwa tatizo kwangu, ukichelewa tu unakuta inakuwa imekula kwako." Mwanafunzi mwingine alituma.

"Mimi nilikuwa nasubiri wakati wa mapumziko kununua bagia, mabumunda, visheti na ubuyu, na 'ice cream', halafu unatemea mate ili usiombwe." Mama mmoja alituma meseji yake.

"Halafu wakati wa kufunga shule, ngumi za kufa mtu lazima umpanie mtu siku ya kufunga kazi yangu ilikuwa kuchora mstari au kushika mchanga ili mtu apite ngumi zianze, du..." Aliandika denti mwingine wa zamani.

"Mimi nakumbuka walimu saa ya matangazo ya kwenda nyumbani, utasikia kesho nataka mje na fimbo, mbolea, maua, miiba, jembe, dumu la maji, majani, sahani ya uji, na enzi hizo ukifaulu darasa la saba yaani mtaa mzima watajua, siku hizi hata ukienda Chuo Kikuu kawaida tu."

"Sisi shuleni kwetu tulikuwa na umoja wa kugawana ice cream." Ni meseji nyingine ya mwanamama, denti wa zamani.

"Kingine ni yale mambo yetu ya mwaka wa mwisho yaani LY, hapa tulikuwa tunajiona wajanja balaa hata mwalimu unamuona kama mwenzio vile. Wakati huo bana we acha tu, kama kungekuwa kurudisha umri nyuma, mimi ningerudisha." Meseji zilikuwa nyingi sana kwa leo tunaishia hapa.

**Tuma meseji 0716 350534**

# Russia yadhibiti eneo lote Mariupol

**LONDON,** UINGEREZA

RAIS wa Russia Vladimir Putin, ametangaza ushindi katika mji wa Mariupol, na kuamuru vikosi vyake kushikilia kila eneo hilo la viwanda ambalo wakati wa vita baridi kulitumika kama ngome kubwa ya nyuklia.

Hata hivyo, wanajeshi wa Ukraine waliosalia ndani ya kiwanda cha chuma , wapiganaji kutoka kikosi cha Azov, baadhi ya wanajeshi wa majini, walinzi wa mpaka na polisi walisema mashambulizi dhidi ya Russia yanaendelea.

Mkuu wa Umoja wa Mataifa wa masuala ya kibinadamu, Martin Griffiths, alisema msafara mpya uko njiani kuelekea kwenye kiwanda kujaribu kuwaondoa raia waliosalia, na unatarajiwa kuwasili mapema.

"Jana kwa ushirikiano uleule na kwa makubaliano yale yale tuliyoyafikia tuliwaokoa zaidi ya raia 340 kutoka sehemu mbalimbali za Mariupol. Hivi tunavyozungumza, msafara unaendelea kufika Azovstal kufikia kesho asubuhi (jana), tunatarajia kuwapokea raia hao waliobaki katika kiwanda hicho chenye giza ambacho wamekaa majuma kadhaa na kuwarudisha kwenye usalama." alisema

Lakini Ikulu ya Kremlin imekanusha kuwa vikosi vyake vilijaribu kuvamia mtambo huo na kusisitiza kuwa eneo lote lenye raia lilikua huru na kulikuwepo na usitishwaji wa mapigano wa siku tatu ulioanza siku ya Alhamisi.

Naibu Waziri Mkuu wa Ukraine Iryna Vereshchuk, alisema kwamba zoezi la uokoaji wa watu huenda likaanza saa sita mchana.

Takriban watoto 20 wanadhaniwa kuwa miongoni mwa raia waliosalia katika kiwanda hicho, huku usambazaji wa chakula na maji ukipungua kwa kasi.

Ujasusi wa Marekani ulisaidia kuizamisha meli ya Russia

MAREKANI inadaiwa kufanikisha meli ya Russia kushambuliwa na kuzamishwa baharini baada ya kutoa taarifa za kijasusi ambazo zilisaidia wanajeshi wa Ukraine kuishambulia kwa makombora.

Kulingana na taarifa zilizotolewa na vyombo vya habari kadhaa vya nchi hiyo, viliwanukuu maofisa ambao hawakutajwa kuwa Ukraine iliiuliza Marekani kuhusu meli iliyokuwa ikisafiri kuelekea kusini mwa Odesa.

Marekani ilisema ilikuwa Moskva na kusaidia kuthibitisha eneo lake. Ukraine kisha iliishambulia kwa makombora mawili.

Pentagon haijatoa maoni. Lakini msemaji wake alisema serikali ilitoa taarifa za kijasusi kuisaidia Ukraine kujilinda.

Maofisa hao ambao awali walisema hawakujua kwamba Ukraine ingeishambulia meli ya Moskva baada ya kusaidia kujua mahali ilipo.

Meli hiyo ya kusafirishia makombora yenye wafanyakazi 510 ilikuwa imeongoza mashambulizi ya wanamaji wa Russia dhidi ya Ukraine, na kuzama kwake lilikuwa pigo kubwa la kijeshi.

Wakati huo, wizara ya ulinzi ya Russia ilisema kwamba risasi zilizokuwemo ndani ya Moskva zilipuka kwa moto usioelezeka na meli hiyo iliyumbayumba ilipokuwa ikivutwa kurudi bandarini.

Vita ya Ukraine imechukua muda mrefu

RAIS wa Belarus, ambaye ni mshirika wa Russia, Alexander Lukashenko, ametetea vita vya Ukraine huku akiashiria kuwa havijapangwa kuendelea muda mrefu.

Ameliambia shirika la habari la AP kwamba operesheni katika nchi ya Ukraine bado itaendelea.

Belarus inapakana na Ukraine na Russia ilituma wanajeshi wakati vita hiyo ilipoanza.

Rais Vladimir Putin wa Russia alimsaidia Lukashenko kubaki madarakani mwaka 2020 baada ya uchaguzi wa marudio wa urais kusababisha maandamano.

Katika mahojiano yake na AP, Lukashenko alisema kuwa kiongozi wa Russia hakuwa na budi ila kuchukua hatua kwa sababu Ukraine inaichokoza .

"Sijazama katika tatizo hili vya kutosha kusema kama linakwenda kulingana na mpango, kama Warussia wanavyosema, au kama ninavyohisi,"alisema

Aliendelea "Nataka kusisitiza kwa mara nyingine ninahisi kama operesheni hii imeendelea."

## Mwanamke mweusi ateuliwa msemaji wa Ikulu Marekani

**KIGALI,** RWANDA

RAIS wa Marekani, Joe Biden amemteua Karine Jean-Pierre kama msemaji wake mpya, na kuwa mtu mweusi wa kwanza kushika nafasi hiyo.

Jean-Pierre, (44), amehudumu kama naibu katibu mkuu wa habari wa utawala huo tangu Biden achaguliwe.

Kuteuliwa kwake inatokana na katibu wa wanahabari Jen Psaki ( 43) kumaliza muda wake, na hivyo kuwa mwanamke mweusi wa kwanza kuongoza idara hiyo ya juu katika Ikulu ya White House.

Makatibu wa vyombo vya habari hutoa taarifa fupi za habari kila siku kwa waandishi wanaofanya kazi Ikulu.

Psaki anajiunga na kituo cha habari cha MSNBC kinachoegemea mrengo wa kushoto.

Kwenye Twitter, Psaki alimtaja mrithi wake kuwa mwanamke wa ajabu na mwenye misingi ya maadili.

"Siwezi kungoja kumuona aking'aa kwani analeta mtindo wake mpya na mzuri kwenye jukwaa," alisema.

## Rais Kagame amsimamisha kazi waziri wa utamaduni

RAIS wa Rwanda, Paul Kagame amemsimamisha kazi waziri wa vijana na utamaduni na kumuweka kizuizi cha nyumbani kutokana na tuhuma ya ufisadi.

Kusimamishwa kwa Edouard Bamporiki, kulitokana na maswala mbalimbali ya uwajibikaji ambayo bado yanachunguzwa, taarifa kutoka ofisi ya wizara hiyo ilisema.

Taarifa hiyo ilieleza kwamba waziri huyo anaendelea kuwa kwenye kizuizi cha nyumbani wakati uchunguzi wake ukiendelea.

Bamporiki, awali alikuwa mfuasi wa Rais Kagame na chama tawala. Hata hivyo amekuwa na ushawishi kwenye mitandao ya kijamii na anachukuliwa kuwa mwanasiasa mwenye utata katika baadhi ya maeneo.

Akiwa mshairi, mtayarishaji wa filamu na mwigizaji maarufu wa tamthilia ya redio, alikuwa kwenye baraza la mawaziri tangu 2019.



Raia wa Sudan wakiandamana kupinga mapinduzi ya serikali pamoja na matumizi ya nguvu za jeshi jana. **PICHA: BBC**

## Mtuhumiwa wa ugaidi nchini Kenya akataa kutoka gerezani

**NAIROBI,** KENYA

KIONGOZI wa dini ya Kiislamu ameiomba mahakama moja ya Kenya kuendelea kubaki gerezani, licha ya kuachiliwa huru kutokana na makosa ya ugaidi yaliyokuwa yakimkabili.

Shekhe Guyo Gorsa Buru, alikamatwa Januari mwaka 2018 kaskazini mwa nchi hiyo na alishtakiwa kwa kuwa na vifaa vya kulitangazia taarifa kundi la kigaidi kwa kushirikiana na wanamgambo wa Al-Shabaab.

Wiki hii mahakama ilimwachilia huru ikisema kuwa serikali imeshindwa kuthibitisha kesi yake.

Hata hivyo alikataa kuondoka katika gereza maarufu la Kamiti akisema anahofia maisha yake.

Muhubiri huyo alidai kuwa anaweza kutekwa nyara na kuuawa na serikali mara tu atakapokuwa huru. Hakimu mkuu aliamuru akae gerezani kwa muda usiozidi siku 30 kisha aachiwe huru.

Hata hivyo atalazimika kuilipa serikali kwa kukaa kwake katika kituo hicho.

Buru amewasilisha kesi tofauti katika mahakama kuu akitaka kupata ulinzi wa serikali pindi atakapoachiliwa.

Ripoti ya hivi majuzi ya Amnesty International na mashirika mengine ya kutetea haki za binadamu ililaumu polisi kwa ongezeko la ukatili na mauaji ya kiholela pamoja na utekaji nyara nchini humo.

## TANGAZO/ HABARI


Air Tanzania
The Wings of Kilimanjaro

# EXCITING CAREER OPPORTUNITY

Air Tanzania Company Limited (ATCL) is making reforms in its structure, internal operations and staffing to accommodate business needs. Therefore, applications are invited from qualified Tanzanians to fill the following vacant position: -

1. **POSITION:** Sales Manager (1 POST)

2. **REPORTING LINE:** Director of Commercial and Business Development

3. **QUALIFICATIONS:**

**The following are qualifications for aspired candidates: -**

- Must have a first Degree in Marketing/Business Administration/Commerce or any business-related field and a Master in Business Administration or relevant field OR;
- A Bachelor Degree in any field with hands on experience in Aviation and a Master Degree in Business Administration or relevant field from a recognized institution.
- Must have at least 8 years' working experience in a competitive and dynamic business environment.
- Hands on skills on airline Commercial Operations is an added advantage

4. **COMPETENCES:**

- High level of integrity, customer focus and good Public Relations skills
- Problem-solving and flexibility
- Decisive, confident and result oriented
- Revenue and cost conscious
- Excellent communication and negotiation skills
- High levels of empathy
- Organizational and time-management skills
- Critical thinking and analytical
- Strong ethical standards

5. **DUTIES AND RESPONSIBILITIES.**

The holder of the position will perform the following duties and responsibilities:

- Develop execute and Drive passenger sales plan guarantee exposure of Air Tanzania's product facilitating delivery of the company's sales targets and business objectives
- Lead, direct, manage, and motivate sales team in order to achieve and ensure maximum sales, based on the growth strategy of Air Tanzania
- Conduct analysis of business environment to facilitate timely response to develop market trend to maximize on opportunities that arise and minimize adverse impact on a company sale
- Ensure product and promotional plan are understood and implemented to the greatest impact on the company sales
- Monitor competitors' activities, evaluate, recommend competitive strategy and pricing level to deliver expected yield, margin and revenue targets.
- Ensure all travelling agents and corporate customers are prioritized, regular visited and professional handled by the sales team to increase revenue and gained market share.
- Identify and allocate resources on what needs to be done by station coordinators/sales executives to cover territory and travel agents effectively
- Manage travel trade relationship, review travel trade developments and suggest appropriate modification in the sales policy to ensure profitability
- Prepare weekly, monthly and annual sales reports
- Provide inputs and participate in the identification and progress of new business opportunity for revenue growth (through special prorate/interline agreements/partnership etc)
- Participate in ATCL's passengers' revenue budget process for the assigned territory
- Assess and propose appropriate incentives schemes to travel agents, corporate travel, and travel trade to enhance productivity, efficiency and maximization of revenue
- Conduct and coordinate annual performance review for all station/sales executives whilst constantly reviewing training development needs skills and abilities
- Resolve operational and reservations issues from travel agent related product or disruption or customer complaints involving individual sales personnel, including addressing any disciplinary problem that may develop within the sales team.
- Develop and monitor expenditure budget/actual and control costs
- Develop and maintain customer profile database and records
- Liaise with marketing and tariffs units and other passengers service-related department of ATCL's to ensure well integrated sales efforts
- Perform any other official duties that may be assigned by supervisor

6. **TERMS AND CONDITIONS:**

Five (5) years contract with remuneration and fringe benefits as per ATCL Scales and Incentive Scheme

7. **MODE OF APPLICATION FOR ALL APPLICANTS:**

Interested applicants must submit a dully signed letter for consideration of the application attached with the following:

i. A detailed curriculum vitae (CV),
ii. Certified copies of all certificates (including secondary school), other relevant certificates, **Applicants who have studied outside Tanzania should have their certificates approved by relevant authorities Tanzania Commission for University (TCU) or National Examination Council-NECTA)**
iii. Two recent passport size photographs
iv. Name and address of at least two reputable referees;
v. Applicant's reliable contact address, email address and telephone number.

**Note: Misrepresentation of qualifications or any other information on application shall warrant legal consequences**

8. **CLOSING DATES:**

Applicants should consider the following closing dates for this post as follows:

Within Fourteen (14) days from the first date of this announcement

The application letters should be directed to the following address: -

**Managing Director and CEO,**
**Air Tanzania Company Limited,**
**P.O. Box 543,**
**DAR ES SALAAM.**

**Date of issue 07/5/2022**


# Awatoa hofu watumishi nyongeza ya mshahara

**Na Mary Geofrey**

Katibu Mkuu wa Chama cha Wafanyakazi wa Serikali za Mitaa Tanzania (TALGWU) amewataka watumishi wa umma nchini kuwa na imani na ahadi ya Rais Samia Suluhu Hassan ya kuongeza mishahara aliyoitoa kwenye sherehe za Mei Mosi mwaka huu.

Rashid Mtima alitoa rai hiyo jana jijini Dar es Salaam wakati akizungumza na waandishi wa habari. Alifafanua:

"Tunamshukuru kwa kutuhakikishia nyongeza ya mishahara, ni muda mrefu sasa watumishi wa umma hawajapandishwa mishahara."

Alimshukuru Rais Samia kwa kusikiliza kilio chao cha muda mrefu kuhusu watumishi walioondolewa kazini kwa vyeti vya kughushi.

Mtima alisema wamekuwa wakiiomba serikali kiliangalia kundi hilo la Watanzania ambao walitumikia kwa uadilifu kwa bahati mbaya wakakutana na tatizo hilo.

"Tunamshukuru Rais kwa kuonyesha upendo mkubwa kwa Watanzania ambao waliitumikia nchi yetu kwa nguvu zao zote hatimaye ameagiza Wizara ya Fedha na Mipango kushughulikia na kuwalipa stahiki zao zinazotokana na makato ya mishahara yao," alisema Mtima.

Alisema wanamshukuru Rais Samia kwa kuagiza mifuko ya hifadhi ya jamii na maofisa utumishi kuhakikisha wanashughulikia haki na stahiki za watumishi wanaotarajia kustaafu ndani ya miezi sita ili inapofika mtumishi anastafu mafao yake yawe tayari.

Kadhalika, alimshukuru Rais Samia kwa kukemea kitendo cha baadhi ya wafanyabiashara kutafuta visingizio na kupandisha kiholela bei za bidhaa na kusababisha ugumu wa maisha.

"Sote tunajua hali ya maisha ni ngumu sana lakini kitendo cha wafanyabiashara kuendelea nao kutukandamiza kwa kuongeza bei ambako kunapunguza uwezo wa mfanyakazi kuweza kununua bidhaa na kukidhi mahitaji yake.

Hivyo, tunamshukuru sana kwa kukemea vitendo hivi," alisema Mtima.

# HADITHI

MGENI wa ajabu anatokea kwenye kijiji cha Semwanza, Lugoba mkoani Pwani. Anakotoka hakujulikani. Watu wote wanamwogopa. Ni kwa sababu hawamjui. Msichana Siwatu anajitolea kumsaidia mgeni huyo. Kwa kufanya hivyo, anabezwa kwa maneno mengi ya kejeli kwa kumsaidia mtu asiyemjua ambaye anaweza kuwa hatari kwa kijiji. Baadhi ya viongozi wa kijiji waliungana na wanakijiji kutaka wamtimue mgeni huyo asiyejulikana, lakini akakataa katakata. Pamoja na kutishwa kuwa atatengwa na kijiji, bado msichana huyo alisimama na msimamo wake ule ule wa kumsaidia kwa sababu alikuwa na shida kubwa. Matokeo ya haya, yanamuingiza Siwatu kwenye msukosuko mkubwa ambao hajawahi kuupata kwenye maisha yake kiasi cha kumkatisha tamaa. Fuatilia kisa hiki.

# KAMA IPO, IPO TU-4

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

Maongezi yao yalikuwa wakati Dibwela na Kobelo wakiwa wametoka nje. Huko nje wakaunda kigenge chao.

"Hivi huyu akitufia hapa tutafanyaje?" Kobelo aliteta na mwenzake.

"We acha tu, ila usiongee hivyo, unakuwa kama unamchuria, tuombee awe na afadhali kesho jioni aondoke, tena tumsindikize wenyewe."

"Kwani mwenyekiti alikwambiaje ulipokwenda kumpa taarifa?"

"Hakuna neno, ila akasema kwa sababu siyo wa kijiji hiki, basi kama atapata nafuu hata kesho basi asindikizwe aondoke, lakini kama bado basi hata kesho kutwa."

"Sasa kama ni hivyo kuna tatizo gani, kwani hata likitokea lolote Serikali ya Kijiji inajua?"

"Kobelo tatizo siyo hilo, ila akitufia huyu mzigo ni wetu, kijiji kinaweza kusiwe na shida na sisi, lakini hasa mimi nitakuwa ndiyo kama msiba wangu, nitagharamikia kama vile ndugu yangu."

"Yote haya kayataka dada yako."

"Kobelo, dada yangu huyu tangu afiwe na wazazi wake, yaani amekuwa na tabia fulani hivi za ajabu. Amekuwa kama mkiwa, huruma imemzidi, kwa hiyo kila kitu akikiona yeye anataka kutoa msaada tu."

"Dada yako bado kidogo tu atakuwa mlokole huyu."

"We acha tu. Ila tufanye hivyo kama tulivyokubaliana, kesho, ikizidi keshokutwa aondoke."

"Sawa."


"Amekunywa uji wote." Alimaka Siwatu kwa furaha. Ni baada ya Dibwela na Kobelo kurudi ndani, wakitoka walikokuwa wanateta.

"Oooh, kweli mgonjwa sasa anaendelea vizuri, nadhani kesho tu anaweza akawa na afadhali zaidi." Akadakia Kobelo.

"Ila bado kidogo kwa sababu akiongea maneno mengi anakohoa, kwa hiyo anatakiwa kupumzika." Akaongeza Siwatu akiwangalia kaka zake kwa zamu.

"Sawa, atalala hapa, kesho tutaangalia hali yake. Nyinyi sasa ondokeni tu, hapa keshafika huyu rafiki yangu. Kobelo, ongozana na dada yangu, mpitishe kwake kwanza, maana imeshakuwa usiku sasa."

Wakati huo Dibwela anaangalia saa kwenye simu yake ya mkononi kiswaswadu, kilichomuonyesha kuwa tayari ni saa tatu usiku.




**"Yaani wameniboa wale. Watu gani hawana hata huruma." Alilalamika. "Bakari utakaa hapa, utaishi hapa siyo mwezi mmoja, muda wowote unaoona kuwa utafaa wewe kuondoka, iwe mwezi, miezi miwili, mitatu sawa tu."**

**************************************

"Nadhani leo umekuwa vizuri zaidi kuliko siku nyingine, unaweza kutuambia kuwa tatizo lilikuwa ni nini?" Lilikuwa ni swali ambalo Dibwela alimuuliza Bakari, siku ya pili baada ya kuonekana hali yake imekuwa nzuri.

"Ni kweli hali yangu ni nzuri, lakini kwa sasa siko vizuri sana kulielezea hilo. Nimesema nitawaeleza lakini siyo sasa."

"Lakini kwa mujibu wa Mwenyekiti wa Kijiji ni kwamba kesho asubuhi au mchana, unatakiwa uwe umeondoka hapa."

Maneno hayo yalimfanya Bakari kukunja uso kwa hofu. Hofu hiyo ilijidhihirisha na Siwatu aliyekuwa akimuonyesha vyombo kaka yake, kuibaini.

"Aaa kaka usiseme hivyo, huyo bado hajapona vizuri bwana, muache."

"Mimi sina ubaya na yeye, na ndiyo maana amekaa hapa kwa siku mbili, ametibiwa, anakula na hata afya yake imeimarika, ila hiyo ni amri kutoka kwa mwenyekiti, siyo mimi." Alijitetea.

"Hapana, huyu atakaa hapa hapa, hadi pale mwenyewe, kwenye nafsi yake akisema anataka kuondoka ataondoka. Kuna siku ataondoka tu, kwani hapa ni kwao? Inawezekana ana familia huyu inayomtegemea, lakini ukiona hivi ujue kuna tatizo linalombabili." Siwatu alimtetea.

Bakari alimuangalia Siwatu. Binti ambaye alimuokoa kwenye kifo, leo anapambana tena kuhakikisha anaendelea kukaa pale akijiuguza, hadi atakapoamua kuondoka mwenyewe.

"Uko sahihi dada yangu. Mimi nilivamiwa na baadhi ya wanakijiji wenzangu huko Msata. Wakanichukua hadi huku Lugoba, wakanipiga na kunitelekeza pale. Wao walidhani kuwa mimi nimekufa. Na hata huko wakienda hawatosema niko wapi. Wao saa hizi wanadhani wameniua na mzoga wangu umeliwa na fisi. Kwa maana hiyo mimi sioni haja ya kwenda kwetu hivi sasa, naomba tu hifadhi ya muda kama mwezi mmoja hivi. Nataka nipumzike na kupanga mkakati wa kwamba hata kama nikirudi nimalize tatizo na lisijirudie tena. Nikirudi nikikuwa dhaifu hivi, maadui zangu watapata nafasi ya kunimaliza tena. Uzuri ni kwamba wanajua nimekufa, kwa hiyo nikikaa muda mrefu watakuwa wamejisahau."

Maneno hayo yaliwaingia Dibwela na dada yake Siwatu. Pamoja na hayo, bado Dibwela alikuwa akiwaza amri ya Mwenyekiti wa Kijiji kuwa mgeni huyo kesho aondoke.

"Kwani hao waliotaka kukuua uliwakosea nini?"

"Ni ugomvi wa mipaka ya mashamba tu dada yangu hakuna kingine."

"Pole sana."

"Ahsante."

Dibwela alikaa kimya. Hakuna cha kuongea tena. Alichofanya ni kwenda kumpitia rafiki yake Kobelo na kwenda kwa Mwenyekiti wa Kijiji.

Amri iliyorudi hapo ni kwamba mgeni aondoke tu, hakuna namna.

"Haendi kokote. Tumemuokoa kwenye kifo, tunashindwaje kumhifadhi tu kwa muda wa mwezi mmoja?" Siwatu akawauliza.

"Siyo mimi dada ni amri ya mwenyekiti nikiikiuka, nitapata adhabu."

"Ni hilo tu au una lingine?" Siwatu aliuliza akionekana kuwa tayari amepandwa na hasira.

"Hilo tu dada."

"Basi atakwenda kukaa kwangu, na hiyo adhabu inipate mimi."

Kilichotokea hapo baada ya maneno hayo, Siwatu alimshika mkono Bakari na kumvuta, akiondoka naye.

Bakari alimfuata nyuma kama mbwa anavyomfuata chatu. Asingeweza kumkiuka mwenyeji wake rasmi, ambaye ndiye ameonekana ni mwokozi wake na amekuwa akiendelea kumpigania na kumtetea kwa nguvu zote. Ulinzi na usalama wake wote ulikuwa mikononi mwake.

Hawakuongea chochote hadi walipofika nyumbani. Alimuachia mkono na kufungua mlango. Akamshika tena mkono na kumuingiza ndani. Bado alionekana amekasirika.

"Yaani wameniboa wale. Watu gani hawana hata huruma." Alilalamika. "Bakari utakaa hapa, utaishi hapa siyo mwezi mmoja, muda wowote unaoona kuwa utafaa wewe kuondoka, iwe mwezi, miezi miwili, mitatu sawa tu."

"Sasa huyo mwenyekiti si hataki, anaweza kukukamata..."

"Siyo kazi yako, hiyo niachie mimi, kama kupewa adhabu, kukamatwa, kuchinjwa, niachie mimi ndiye nitakayejua hilo." Alijibu akionekana bado ana hasira.

Taarifa za Siwatu kumhifadhi mtu aliyeokotwa majeruhi kwenye kijiji hicho zilifika kwa Mwenyekiti wa Kijiji. Yeye alitaka aondoke baada ya siku tatu. Hakutaka kutoa adhabu yoyote kutokana na historia ya binti mwenyewe. Ni yatima na jinsi alivyoondokewa na wazazi wake, kila mtu anajua na wengi wamekuwa wakimuonea huruma. Licha ya yote hayo, hakuwa binti mwenye mambo mengi. Alikuwa na akili, nidhamu na adabu, hivyo alihofia kufanya maamuzi ya peke yake.

Akaitisha kikao cha kijiji kumjadili. Kumjadili Siwatu aliyekiuka sheria, kanuni na utamaduni uliowekwa na kijiji hicho cha Semwanza.

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

# AZAM YAIKARIBISHA KMC LIGI KUU BARA BILA HOFU

**Na Saada Akida**

RAUNDI ya 22 ya Ligi Kuu Tanzania Bara inatarajia kuendelea leo katika viwanja vitatu tofauti hapa nchini ambapo Azam FC itawakaribisha KMC FC, mechi itakayochezwa kuanzia saa 1:00 usiku kwenye Uwanja wa Azam Complex, uliopo Chamazi nje kidogo ya Dar es Salaam.

Mechi nyingine za ligi hiyo zitakuwa ni kati ya Geita Gold FC dhidi ya Kagera Sugar itakayopigwa kwenye Uwanja wa Nyankumbu kuanzia saa 8:00 mchana wakati Mtibwa Sugar itawaalika Mbeya City kwenye Uwanja wa Manungu uliopo Turiani, Morogoro.

Mechi hizo zinahusisha timu ambazo ziko katika vita ya kutaka nafasi ya tatu na ya nne ambazo ni Namungo FC , Azam FC, Kagera Sugar, Mbeya City na Geita Gold.

Mtibwa Sugar wao wanapambana kusaka pointi katika mchezo wao ili kujiweka katika nafasi nzuri ya kujiondoa katika hatari ya kushuka chini katika nafasi ya 10 ikiwa na pointi 24.

**Baadhi ya makocha wakizungumzia maandalizi kuelekea mechi hizo, Mwalimu wa KMC FC, Thierry Hitimana, alisema wachezaji wake wako tayari kwa ajili ya kutafuta alama muhimu katika mchezo wao dhidi ya Azam FC.**

"Tumejiandaa vizuri kwenda kutafuta pointi muhimu katika mchezo huo, natambua Azam FC iko vizuri, tayari wachezaji wangu wako tayari kwa ajili ya kutafuta matokeo ya kuhakikisha timu inajinasua katika nafasi ya chini ya msimamo," alisema Hitimana.

Katika mechi hiyo, KMC FC itawakosa wachezaji wawili, Awesu Awesu na Iddi Kipagwile ambao ni majeruhi na waliondolewa katika mipango ya mchezo huo.

Naye Kocha wa Makipa wa Azam FC, Iddi Abubakar alisema malengo makubwa katika mchezo wa leo ni kutafuta pointi tatu ili kujiweka katika nafasi nzuri katika msimamo.

"Tumerejea nyumbani baada ya kumaliza mechi mbili na kupata pointi moja na sasa tumerudi na nguvu zetu, tunaenda kupambana kusaka alama muhimu katika mchezo huo," alisema Iddi.

Kuelekea mchezo wa 170, kati ya Mtibwa Sugar dhidi ya Mbeya City, Kocha Mkuu wa Mbeya City, Mathias Lule alisema mechi hiyo itakuwa na ushindani mkubwa kwa sababu kila upande unahitaji pointi muhimu zitakazowafikisha katika malengo yao.

"Mechi itakuwa nzuri na ushindani kwa sababu wapinzani wetu wako katika nafasi ya chini na wanahitaji matokeo kujiondoa huko, hata sisi pia tunatakiwa pointi ili kujiweka katika nafasi nzuri ya kuhitaji nafasi nne za juu," alisema Lule.



Wanariadha wa mbio za mita 1,500 wakichuana katika mbio za Mbeya Tulia Marathoni (MTM) zilizofanyika kwenye Uwanja wa CCM Sokoine jijini Mbeya jana. Kilele cha mbio hizo kitafanyika leo kwa wanariadha kuchuana katika umbali wa kilomita 10, nusu marathoni na marathoni. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mbeya Tulia Marathoni yatikisa

**Mwandishi Wetu,** MBEYA

WANARIADHA kutoka sehemu mbalimbali nchini jana walionyeshana uwezo wao katika ufunguzi wa mbio za kwanza za Mbeya Tulia Marathoni (MTM) zinazofikia tamati leo kwenye Uwanja wa Sokoine jijini hapa, chini ya uratibu wa Taasisi ya Tulia Trust na kudhaminiwa na wadau mbalimbali ikiwamo benki ya CRDB na wauzaji wa gezi ya ORYX.

Msimu mpya wa tano wa mbio hizo ulifunguliwa kwa wanariadha kuchuana katika mbio za mita 100, 200, 400, 800 na 1500 huku leo wanariadha watapambana katika mbio za kilomita tano, kilomita 10, kilomita 21 na kilomita 42, zikiongozwa na Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano, Dk. Tulia Ackson. Katika mbio za mita 100 kwa upande wa wanaume, nyota wa timu ya taifa, Ally Gulam alitwaa dhahabu huku Magdalena Shauri aliibuka kinara akimpiku Jackline Sakilu wa timu ya taifa aliyemaliza wa pili katika mbio za kilomita 1,500.

Magdalena aliibuka kinara baada ya kutumia dakika 4:33:21, Sakilu alimaliza wa pili akitumia dakika 4:34:45 na Marcelina Mbua alihitimisha tatu bora.

Kwenye mbio za mita 800, Saimon Msonjo alimpiku Andrew Rhobi wa timu ya taifa baada ya kuchomoka kutoka nyuma ikiwa ni mita 200 kabla ya kumaliza mbio hiyo na kumpita Rhobi ambaye alimaliza wa pili.

Kwenye fainali ya wanawake, Sakilu alikuwa bingwa akitumia dakika 2:17:90, Aisha Magelani alimaliza wa pili akitumia dakika 2:24:61 na Gaudencia Paulo alihitimisha tatu bora akitumia dakika 2:25:12.

Meneja wa Tulia Trust, Jackline Boaz alisema washindi wa kwanza hadi wa tatu kwenye mbio za uwanja wamezawadiwa medali na fedha taslimu na wale wa mbio za barabarani leo wataondoka na zawadi kama hizo.

"Tumetenga zaidi ya Sh, milioni 30 kwa mabingwa," alisema Jackline.

## Shomari akamilisha hesabu za ubingwa

**Na Saada Akida**

BEKI wa Yanga, Kibwana Shomari amesema safu ya ulinzi ya timu hiyo imejipanga kuendelea kujituma na kupambana ili kufikia malengo waliyojiwekea katika msimu huu wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Akizungumza na gazeti hili jana, Shomari alisema licha ya kuambulia pointi mbili katika michezo miwili iliyopita nia yao ni kupata ushindi katika michezo iliyobakia ya ligi hiyo.

Shomari alisema bado hawajaridhika na pointi walizonazo na wanahitaji kuwaacha kwa tofauti ya pointi nyingi wapinzani wao wanaowakimbiza.

"Kikubwa mpaka sasa, hatuhitaji kupoteza mchezo wowote na ili tusipoteze tunahitaji kucheza mechi bila kuruhusu bao kwa kila mchezo, sisi safu ya ulinzi tupo tayari kwa ajili ya kupambana kutimiza malengo," alisema Shomari.

Aliongeza ligi imekuwa na ushindani mkubwa na kila timu inajipanga vizuri kwa ajili ya kujiweka katika nafasi salama hasa katika timu ambazo watakutana nazo hivi karibuni.

Yanga imebakiwa na michezo nane kati ya hiyo inahitaji kushinda mitano ili kutangaza ubingwa msimu huu bila ya kuangalia matokeo ya timu nyingine yoyote.

Mechi zilizobakia ni dhidi ya Tanzania Prisons, Dodoma Jiji, Mbeya Kwanza, Biashara United, Coastal Union, Polisi Tanzania, Mbeya City na Mtibwa Sugar.

## Magereza, Jeshi Stars majaribuni

**Na Saada Akida**

TIMU 10 za mchezo wa wavu zinatarajia kushuka dimbani wikiendi hii kuwania ubingwa wa Mkoa wa Dar es Salaam, mechi zote zikipangwa kuchezwa kwenye Uwanja wa Ndani wa Benjamin Mkapa jijini, imeelezwa.

Ligi hiyo inayochezwa kwa mfumo wa nyumbani na ugenini inaandaliwa na kusimamiwa na Chama cha Wavu Mkoa wa Dar es Salaam (DAREVA).

Mechi ya kwanza kwa upande wa wanawake itakuwa ni kati ya JKT dhidi ya UDSM wakati Star Girls watawavaa Chui.

Kwa wanaume, Kigamboni itacheza dhidi ya Twalipo, JTK Watches dhidi ya KIUT na mchezo wa mwisho kati ya Chui dhidi ya UDSM.

Ligi hiyo itaendelea tena kesho na kwa wanawake KIUT watachuana na Wazo wakati Jeshi Stars itawakabili Magereza na kwa wanaume leo Jeshi Stars watashuka kuivaa Wazo huku Tanesco watapimana na Nyika.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### GUARDIOLA KUBAKI CITY

KOCHA, Pep Guardiola atatia saini mkataba mpya na Manchester City ili kubakia katika Uwanja wa Etihad hadi mwaka 2025 baada ya kuiambia klabu hiyo ana ari zaidi ya kuishindia taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya. (***Star***)

### DE JONG KUTUA CITY

MANCHESTER City inafikiria kumnunua kiungo wa kati wa Timu ya Taifa ya Uholanzi, Frenkie de Jong mwenye umri wa miaka 25 ili kuiimarisha klabu hiyo msimu ujao. (***Mail***)

### PICKFORD KUWEKWA SOKONI

KLABU ya Everton imejiandaa kumuuza kipa, Jordan Pickford mwenye umri wa miaka 28, ili kuchangisha fedha za kuijenga upya timu hiyo. Tottenham na Newcastle zinachunguza hali ya mlinda mlango huyo wa England. (***Talksport***)

### TORRES ANUKIA SPURS

MAOFISA wa Tottenham Hotspur waliwatazama wachezaji wawili wa Villareal katika mechi yao ya nusu fainali waliyopoteza siku ya Jumanne, - beki wa kati Pau Torres na Arnaut Danjuma, wote wana umri wa miaka 25. (***90 Min***)

### TRAORE AGEUKA LULU

KLABU za Leeds na Tottenham Hotspurs zina nia ya kumsajili winga wa Wolves na Hispania, Adama Traore. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26 kwa sasa yuko Barcelona kwa mkopo, lakini klabu hiyo ya Hispania haitarajii kumsajili kwa mkataba wa kudumu. (***Team Talk***)

### OSIMHEN AICHAGUA ARSENAL

MSHAMBULIAJI wa Napoli na Nigeria, Victor Osimhen mwenye umri wa miaka 23 amesema angependelea kujiunga na Arsenal badala ya Manchester United au Newcastle (***Gazzetta dello Sport, via Express***)

### DYBALA KUTUA DORTMUND

NYOTA anayewaniwa na Arsenal na Manchester United, Paulo Dybala amepata ofa ya kujiunga na Borussia Dortmund wakati mkataba wa mshambuliaji huyo wa Argentina unakamilika mwisho wa msimu huu. (Corriere dello Sport)

### MBAPPE, PSG NJIA NYEUPE

KYLIAN Mbappe anakaribia kuongeza mkataba wake kwa miaka miwili na mabingwa wa Ufaransa PSG ambao utagharimu pauni milioni 42.5 kwa mwaka kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23. (***Le Parisien***)

### RB YAMBAKISHA NKUNKU

KLABU ya RB Leipzig inataka mchezaji anayelengwa na Manchester United, Christopher Nkunku mwenye umri wa miaka 24 kubakia kwa msimu mmoja zaidi. (***Bild***)

### BAILLY KUONDOKA UNITED

MLINZI wa kati wa Manchester United na raia wa Ivory Coast, Eric Bailly mwenye umri wa miaka 28 pamoja na beki wa England, Phil Jones (30), wote wamewaambia wachezaji wenzao katika klabu hiyo wataondoka mwisho wa msimu huu. (***Manchester Evening News***)

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# MAMA AKATAA MBAPPE KUSAINI MKATABA PSG

## ●●● Asema mazungumzo kuhusu hatima yake yanaendelea kwa utulivu ili...

**PARIS,** Ufaransa

KYLIAN Mbappe bado hajakubaliana na Paris Saint-Germain kuhusu kusaini mkataba mpya wala klabu nyingine yoyote, kwa mujibu wa mama mzazi wa nyota huyo wa Ufaransa.

Huku mkataba wa sasa wa Mbappe ukitarajiwa kukamilika mwezi ujao, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23 amekuwa akihusishwa anataka kuhamia Real Madrid.

Mbappe amefunga mabao 35 na kutoa pasi za mabao 19 kwa timu hiyo inayonolewa na Mauricio Pochettino katika mashindano yote msimu huu.

PSG walishinda taji la Ligi Kuu Ufaransa, Ligue 1, lakini walishindwa dhidi ya Madrid kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya katika hatua ya mtoano hapo Machi.

**Gazeti la Ufaransa Le Parisien liliripoti kwenye tovuti yake siku ya Alhamisi kwamba Mbappe alikuwa karibu kufikia makubaliano ya kuongeza muda wake wa kukaa hapo Paris hadi Juni, mwaka 2024.**

Fayza Lamary, mama yake Mbappe ambaye ni mshindi wa Kombe la Dunia mwaka 2018, amekanusha mapendekezo ambayo Mbappe ameamua kuhusu mustakabali wake.

"Hakuna makubaliano kimsingi na Paris Saint-Germain (au klabu nyingine yoyote)," aliandika Lamary kupitia ukurasa wake wa Twitter.

"Majadiliano kuhusu mustakabali wa Kylian yanaendelea katika hali ya utulivu mkubwa ili kumruhusu kufanya chaguo bora, kwa heshima ya pande zote."

Mbappe alifunga mabao yake ya 130 na 131 katika maisha yake ya Ligue 1 katika mechi yake ya mwisho wakati PSG ilipotoka sare ya 3-3 na Strasbourg, na kumfanya kuwa mfungaji bora wa pili katika michuano hiyo karne hii baada ya Edinson Cavani, aliyefunga mara 138 kwenye ligi akiwa na kikosi cha Paris.

LIVE IN PLAY
CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 1,224

MECHI KALI
LIVERPOOL
VERSUS
TOTTENHAM
1 | 1.45
X | 4.66
2 | 5.75

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa




# PELE AMWAGA SIFA KWA RODRYGO

**SAO PAULO,** Brazil

RODRYGO amepongezwa na gwiji wa soka wa Brazil, Pele kwa mchango wake katika ushindi wa ajabu wa mabao 6-5 waliopata Real Madrid dhidi ya Manchester City katika nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Akiwa amechukua nafasi ya Toni Kroos akitokea benchi dakika ya 68 muda mfupi kabla ya bao la Riyad Mahrez kuwaweka Madrid nyuma kwa 5-3, Rodrygo alifunga bao la dakika za mwisho na kulazimisha mchezo huo kwenda dakika za nyongeza, ambapo penalti ya Karim Benzema iliwapeleka Los Blancos hao fainali.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 21 amekuwa mchezaji wa kwanza kufunga mabao mawili dakika ya 90 katika mchezo wa mtoano wa Ligi ya Mabingwa Ulaya, na mchezaji wa pili tu kufunga mabao mawili katika nusu fainali katika michuano hiyo, baada ya Georginio Wijnaldum wa Liverpool dhidi ya Barcelona katika msimu wa 2018-19.

Baada ya kubadilisha mwendo wa sare kwa kufunga mabao mawili ndani ya sekunde 91, Rodrygo, ambaye amecheza mechi tano kwa Brazil, alipokea sifa nyingi kutoka kwa mtani wake mashuhuri kwenye mitandao ya kijamii, Pele.

"Siku zote nilijua siku ya kukupongeza ingekuja rafiki yangu," aliandika Pele kwenye ukurasa wake wa Instagram, sambamba na picha yake na Rodrygo akiwa amevalia jezi ya Brazil.

"Hakuna njia nyingine kwa wale wanaofanya kazi kwa bidii na kupenda wanachofanya. Utatuletea furaha nyingi, hongera. Siwezi kungoja kutazama fainali!"

Rodrygo alifunga bao lake la kwanza la kimataifa katika ushindi wa mabao 4-0 dhidi ya Paraguay, Februari mwaka huu na amefunga magoli nane na kutoa asisti nane katika msimu wenye mafanikio akiwa na Madrid, ambayo ameanza mara 21 katika mashindano yote.

Madrid itamenyana na Liverpool katika fainali yao ya 17 ya Kombe la Ulaya maarufu Ligi ya Mabingwa Ulaya baadaye mwezi huu.

Los Blancos sasa wameingia fainali angalau mara sita zaidi ya klabu nyingine yoyote, na waliwashinda Liverpool katika mechi yao ya mwisho kama hii mwaka 2018.

# *Dybala sasa rasmi kuondoka Juventus*

**TURIN,** Italia

MKATABA wa Paulo Dybala na Juventus unamalizika mwishoni mwa msimu huu na kuna taarifa tayari amefanya uamuzi kuhusu wapi anataka kuelekea.

Atletico Madrid na Barcelona zote zimekuwa zikitajwa mara kadhaa kuhitaji huduma ya Dybala, mchezaji wa kimataifa wa Argentina.

Kwa mujibu wa Gazzetta dello Sport kama ilivyoainishwa na Marca, mshambuliaji huyo hataondoka Italia.

Taarifa inataja nyota huyu atajiunga na wapinzani wakali wa Juventus ambao ni Inter Milan.

Dybala atasaini mkataba wa miaka minne pale San Siro wenye thamani ya euro milioni sita kwa mwaka.

Dybala ameichezea Juventus mechi 289, akichangia mabao 114 na asisti 48. Ameshinda Scudetto mara tano, Coppa de Italia mara nne na Supercoppa Italiana mara tatu.

Dybala anatumaini uhamisho wake katika majira ya joto unaweza kumkuza kwenye kikosi cha Argentina cha Kocha, Lionel Scaloni kuelekea fainali za Kombe la Dunia mwaka huu.

Argentina wakiongozwa na Lionel Messi wataelekea Qatar.



4,601,040

# JACKPOT
## MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 07/05/22 | 17:00 | Burnley vs Aston Villa | 2.87 | 3.17 | 2.41 |
| 02. 07/05/22 | 17:00 | Brentford vs Southampton | 2.21 | 3.37 | 3.02 |
| 03. 07/05/22 | 19:00 | Sassuolo vs Udinese | 2.25 | 3.56 | 2.82 |
| 04. 07/05/22 | 19:30 | Brighton vs Manchester Utd | 2.62 | 3.21 | 2.58 |
| 05. 07/05/22 | 19:30 | Hertha BSC vs Mainz | 2.52 | 3.31 | 2.62 |
| 06. 07/05/22 | 20:00 | Benfica vs Porto | 2.74 | 3.43 | 2.39 |
| 07. 08/05/22 | 16:00 | Leicester vs Everton | 2.31 | 3.22 | 2.97 |
| 08. 08/05/22 | 16:00 | Venezia vs Bologna | 2.93 | 3.27 | 2.31 |
| 09. 08/05/22 | 17:15 | Villarreal vs Sevilla FC | 2.30 | 3.25 | 3.05 |
| 10. 08/05/22 | 17:45 | Feyenoord vs PSV Eindhoven | 2.41 | 3.62 | 2.58 |
| 11. 08/05/22 | 19:00 | Salernitana vs Cagliari | 2.35 | 3.26 | 2.87 |
| 12. 08/05/22 | 19:30 | Espanyol vs Osasuna | 2.59 | 3.14 | 2.74 |
| 13. 08/05/22 | 22:00 | Atletico Madrid vs Real Madrid | 2.37 | 3.30 | 2.90 |

## MECHI ZA USHINDI

“1” - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
“X” - NI TIMU KUTOKA SARE
“2” - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

## JUMAMOSI - 07/05/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:00 | 1190 | Celtic vs Hearts | 1.26 | 5.76 | 9.14 |
| 14:00 | 4750 | Geita Gold FC vs Kagera Sugar | 2.42 | 2.59 | 3.32 |
| 14:30 | 1022 | Hull City vs Nottingham | 4.26 | 3.47 | 1.79 |
| 14:30 | 2460 | Huddersfield vs Bristol City | 1.91 | 3.52 | 3.67 |
| 14:30 | 2739 | Luton Town vs Reading | 1.47 | 4.26 | 6.14 |
| 14:30 | 3236 | West Bromwich vs Barnsley | 1.37 | 4.74 | 7.11 |
| 14:30 | 5912 | Preston vs Middlesbrough | 4.76 | 3.82 | 1.65 |
| 15:00 | 3237 | Mallorca vs Granada | 1.95 | 3.35 | 3.85 |
| 16:00 | 5745 | Torino vs Napoli | 3.43 | 3.43 | 2.02 |
| 16:30 | 2344 | Zenit St Petersburg vs FK Khimki | 1.21 | 6.12 | 10.85 |
| 16:30 | 2441 | Hoffenheim vs Bayer Leverkusen | 3.13 | 3.92 | 1.98 |
| 16:30 | 2567 | Greuther Furth vs Borussia Dortmund | 7.73 | 5.75 | 1.29 |
| 16:30 | 2700 | FC Koln vs VfL Wolfsburg | 1.58 | 4.28 | 4.68 |
| 16:30 | 3579 | SC Freiburg vs Union Berlin | 1.87 | 3.62 | 3.71 |
| 17:00 | 1878 | Chelsea vs Wolverhampton | 1.33 | 4.76 | 8.53 |
| 17:00 | 2055 | Burnley vs Aston Villa | 2.88 | 3.18 | 2.39 |
| 17:00 | 2271 | Ross County vs Motherwell | 2.30 | 3.17 | 3.07 |
| 17:00 | 4900 | Brentford vs Southampton | 2.14 | 3.37 | 3.17 |
| 17:00 | 5216 | Crystal Palace vs Watford | 1.62 | 3.81 | 4.95 |
| 17:15 | 2925 | Athletic Bilbao vs Valencia | 1.55 | 3.95 | 5.80 |
| 17:30 | 3521 | GD Estoril vs Moreirense | 2.55 | 3.20 | 2.70 |
| 18:00 | 2795 | Brest vs Strasbourg | 4.39 | 3.69 | 1.74 |
| 18:00 | 2835 | Amazulu vs Sekhukhune United | 2.20 | 2.87 | 3.61 |
| 18:00 | 3950 | Stellenbosch vs Maritzburg Utd | 2.08 | 2.78 | 4.17 |
| 19:00 | 2099 | Adana Demirspor vs Alanyaspor | 1.97 | 3.63 | 3.43 |
| 19:00 | 3093 | FC Lugano vs BSC Young Boys | 3.93 | 3.68 | 1.82 |
| 19:00 | 3271 | Basaksehir vs Galatasaray | 1.95 | 3.48 | 3.63 |
| 19:00 | 5040 | Sassuolo vs Udinese | 2.29 | 3.62 | 2.73 |
| 19:00 | 5446 | CSKA Moscow vs Sochi | 2.15 | 3.46 | 3.07 |
| 19:30 | 3153 | Hertha BSC vs Mainz | 2.42 | 3.36 | 2.71 |
| 19:30 | 3346 | Brighton vs Manchester Utd | 2.66 | 3.20 | 2.55 |
| 19:30 | 3562 | Cadiz CF vs Elche | 1.72 | 3.50 | 4.91 |
| 19:30 | 5276 | Celta Vigo vs Alaves | 1.86 | 3.40 | 4.20 |
| 19:45 | 3038 | Twente vs Fortuna Sittard | 1.39 | 4.66 | 6.93 |
| 20:00 | 3626 | Benfica vs Porto | 3.03 | 3.43 | 2.21 |
| 20:00 | 5777 | Banik Ostrava vs Hradec Kralove | 2.15 | 3.38 | 3.33 |
| 20:30 | 4001 | Cape Town City vs TS Galaxy FC | 1.89 | 3.17 | 4.25 |
| 21:00 | 4581 | Willem II Tilburg vs Heracles Almelo | 2.21 | 3.22 | 3.17 |
| 21:00 | 4880 | Wisla Krakow vs Jagiellonia | 1.87 | 3.46 | 3.61 |
| 21:00 | 5699 | PEC Zwolle vs Utrecht | 2.73 | 3.33 | 2.42 |
| 21:30 | 2870 | St. Gallen vs FC Zurich | 2.18 | 3.69 | 2.89 |
| 21:45 | 3775 | Lazio vs Sampdoria | 1.42 | 4.67 | 6.16 |
| 21:45 | 5383 | Liverpool vs Tottenham | 1.45 | 4.66 | 5.75 |
| 21:45 | 5962 | KAA Gent vs Mechelen | 1.48 | 4.38 | 5.78 |
| 22:00 | 3639 | Groningen vs Sparta Rotterdam | 2.06 | 3.27 | 3.47 |
| 22:00 | 5119 | Betis vs Barcelona | 2.91 | 3.50 | 2.27 |
| 22:00 | 5199 | Nice vs Nantes | 2.06 | 3.34 | 3.44 |
| 22:30 | 1467 | Portimonense vs Sporting Lisbon | 7.56 | 4.67 | 1.37 |
| 22:30 | 5164 | Charlotte FC vs Inter Miami CF | 1.72 | 3.74 | 4.75 |
| 23:00 | 2021 | Montreal Impact vs Orlando City | 2.02 | 3.50 | 3.60 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.




# KASANGA ALAMBA MILIONI 50.5 JACKPOT BONUS YA SPORTPESA

**Na Mwandishi Wetu**

MKAZI wa Sombetini jijini Arusha, Ezra Kasanga, ameshinda Sh. milioni 50.5 katika Jackpot Bonus ya Sportpesa iliyochezwa mwishoni mwa wiki iliyoisha baada ya kupatia ubashiri kwa usahihi mechi 12 kati ya mechi 13.

Akizungumza baada ya hafla ya makabidhiano ya mfano wa hundi katika ofisi za Sportpesa jijini Dar-es-Salaam, Ezra, ambaye pia ni mwajiriwa wa Serikali na mjasiriamali alisema alianza kucheza na Sportpesa miaka minne iliyopita.

“Nilianza kucheza na Sportpesa mwaka 2018 baada ya kuona matangazo katika mitandao na pia baadhi ya washikaji zangu walikuwa wanacheza sana, hivyo kunivutia na mimi kufuata nyayo zao.”

Aliongeza tangu ameanza kucheza alishawahi kushinda Sh. milioni tano siku za nyuma na hivyo kupata moyo wa kuendelea.

**“Siku za nyuma mwaka mmoja na ushehe nilishinda Sh. milioni tani a ushehe kwenye malti beti”.**

Kuhusu mkeka wake ulioshinda Jackpot anasema aliona mechi siku ya Jumatatu iliyopita na alijipa siku tano akiuchambua mpaka siku ya Jumamosi iliyopita ndipo alipoweka ubashiri wake.

“Niliweka mkeka mmoja tu ambao niliuchagua kwa umakini kwa siku tano”. Anamalizia kwa kusema alikuja kujua kashinda siku ya Jumapili usiku wakati yupo nyumbani kwake anaangalia mechi ya Simba dhidi ya Orlando Pirates.



“SMS iliingia ikinipa hongera kwa kushinda jackpot bonus. Nilimwambia mke wangu, lakini hakuamini kama ushindi wa kiasi hiki ulikuwa ni taarifa ya kweli. Bahati nzuri sms ya kiwango cha fedha nayo iliingia baada ya muda sio mrefu hivyo tulifurahia kwa pamoja”.

Ezra anawashauri Watanzania waiamini Sportpesa na pia wasiishi kwa kusikiliza maneno ya mitaani, kwamba mchezo huu ni wa kitapeli.

“Mimi ni shuhuda, hii pesa niliyoshinda nitaongeza kwenye biashara yangu ya Bajaji na pia kiasi kingine nitaangalia nini cha kufanya siku za mbeleni”.

Akizungumza kwa niaba ya Sportpesa Meneja Uhusiano na Mawasiliano, Sabrina Msuya alimpongeza Ezra kwa ushindi huo wa Jackpot bonus na kuwataka Watanzania kuendelea kucheza kwani wiki hii Jackpot imesimamia Sh. bilioni 1.9.




# Uchovu chanzo Biashara kulala

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Dodoma Jiji, Masoud Djuma, amesema anaamini wameifunga Biashara United katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa juzi kwenye Uwanja wa Nyamagana jijini Mwanza kutokana na uchovu waliokuwa nao wenyeji wao na si vinginevyo.

Biashara United ilishuka dimbani hapo Jumatatu kuikabili Mtibwa Sugar na mchezo huo ulimalizika kwa sare ya bao 1-1.

Masoud alisema timu zote mbili zilicheza mpira unaofanana na mfumo unaoshabihiana kutokana na makocha wote kufahamiana.


“Tunajuana sisi, nashukuru nimekutana na ndugu yangu, miaka mingi hatujaonana, yeye alitaka kutulazimisha kucheza mpira nyuma, yaani tuzuie, wote wawili mpira wetu ni wa aina moja, wa kucheza, mimi nikakataa kunisukuma, nikalazimisha na mimi nishambulie, wote tucheze mbele. Tatizo lao ni kwamba Biashara United wameumizwa na uchovu, “ alisema kocha huyo ambaye alikutana na Mrundi mwenzake, Vivier Bahati.

Aliongeza mechi hiyo imekwisha na sasa wanakwenda kujiandaa kukutana na Coastal Union, mchezo ambao pia unatarajiwa kuwa na ushindani kutokana na nafasi waliyopo wenyeji hao wa jiji la Tanga.

# Michezo

Nipashe Jumamosi Mei 7, 2022



Mama akataa Mbappe kusaini mkataba PSG

UKURASA 21




Beki wa kimataifa wa Simba, Henock Inonga akiwa ameshika tuzo na zawadi ya hundi ya Sh. milioni mbili alizokabidhiwa baada ya kuibuka mshindi wa Tuzo ya Mchezaji Bora wa mashabiki wa Aprili. Tuzo hiyo hutolewa na Kampuni ya Emirate Aluminium ACP. **PICHA: SIMBA SC**

# Nabi amwaga 'sumu' Yanga

## ●●● Awataka wachezaji kutobweteka katika dakika za majeruhi ili...

**Na Saada Akida**

ILI kuhakikisha wanafikia malengo, Kocha Mkuu wa Yanga, Nesreddine Nabi amezidisha ukali kwa wachezaji wake ambapo amewataka kupambana na kufikiria kama wanaanza msimu ili kupata matokeo mazuri katika michezo yao nane iliyobakia ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

Katika mechi hizo nane zilizobakia, Yanga ambao ndio vinara inahitaji kushinda michezo mitano ili kutangazwa mabingwa wapya wa msimu huu bila ya kuangalia matokeo ya timu nyingine yoyote.

Michezo iliyobaki ni dhidi ya Tanzania Prisons, Dodoma Jiji, Mbeya Kwanza, Biashara United, Coastal Union, Polisi Tanzania, Mbeya City na Mtibwa Sugar.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Nabi alisema ameamua kubadili fikra zao baada ya kuona wachezaji wake wanaonekana kuridhika au wakiamini wameshamaliza kazi kutokana na namna walivyocheza katika michezo miwili iliyopita dhidi ya Simba na Ruvu Shooting.

Nabi alisema bado hawajafikia malengo ya kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara na baada ya kutoka suluhu na Simba wachezaji wakawa wameridhika jambo ambalo halijamfurahisha.

"Wachezaji wanatakiwa kujitoa na kupambana zaidi ya hapo, lengo ni kutwaa ubingwa wa ligi, sitaki kuona mchezaji yoyote anacheza kwa kuridhika na kuondoa ule ubora wake aliokuwa nao kabla ya mchezo dhidi ya Simba," alisema Nabi.

**Alisema anahitaji wachezaji kujitoa zaidi katika michezo iliyobaki ili kuzipata pointi hizo wanazozihitaji ambazo hazitafikiwa na timu yoyote katika mbio hizo za kuwavua ubingwa wapinzani wao, Simba.**

Kocha huyo alisema wanahitaji kuweka rekodi nyingine ikiwamo kuchukua ubingwa kwa idadi kubwa ya pointi na mabao mengi ya kufunga pia ikiwezekana wamalize msimu bila ya kupoteza mechi hata moja.

"Baada ya kurejea jijini, tutarudi uwanjani kwa ajili ya kufanyia kazi mapungufu yaliyojitokeza katika michezo miwili iliyopita na kujiweka sawa na mechi iliyopo mbele yetu dhidi ya Tanzania Prisons," alisema kocha huyo.

Yanga itashuka tena dimbani keshokutwa kuwakaribisha Tanzania Prisons wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

Wakati huo huo, Ligi Kuu Tanzania Bara inatarajiwa kuendelea tena leo kwa Geita Gold FC kuwakaribisha Kagera Sugar wakati Mbeya City wameifuata Mtibwa Sugar kwenye Uwanja wa Manungu, Turiani mkoani Morogoro huku Azam FC ikiwaalika KMC kwenye Uwanja wa Azam Complex jijini.

Simba iliyoko katika nafasi ya pili kwenye msimamo wa ligi hiyo ndio mabingwa watetezi lakini pia vita ivingine ngumu ikionekana iko chini kwa timu zinazotakiwa kujinusuru na janga la kushuka daraja.

# Simba Sc yawaamsha mashabiki 2021/22

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI msimu wa Ligi Kuu Tanzania Bara ukiwa unaelekea ukingoni, Meneja Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally ameibuka na kusema kama timu 14 kati ya 16 zinaweza kushuka daraja, basi ligi hiyo ni dhaifu.

Akizungumza kama mdau wa michezo, Ahmed alisema hatua ya timu 14 kushindana kubaki katika Ligi Kuu Tanzania Bara na si kutwaa ubingwa, basi kuna shida mahali na inapaswa jambo hili lifanyiwe kazi kwa mustakabali wa maendeleo ya soka la Tanzania.

"Katika timu 16, timu 14 zinaweza kushuka daraja, hii sio aina ya ligi tunayoihitaji haiwezekani timu nyingi zigombanie kushindwa.

Ligi yenye ushindani ni ile ambayo timu nyingi zinagombania ubingwa, timu nyingi msimu huu zimekua dhaifu, tupo raundi ya 22 lakini ni timu tatu tu zimefikisha pointi angalau 30. Msimu uliopita hadi kufika raundi ya 22, timu saba zilikua na pointi angalau 30.

Hii ni hatari kwa sababu bingwa anaweza kupatikana kwa kufunga wadhaifu wengi. Najua utauliza kwanini na wewe usiwafunge hao dhaifu wengi ili uwe bingwa, ukweli ni kwamba katika hizo mechi zetu dhidi ya timu dhaifu nasi tulifanya udhaifu," alisema Ahmed.

Aliongeza maoni yake hayo hayana uhusiano wowote na Simba kukosa ubingwa au kupata ubingwa msimu huu, bali ni kuangalia na maendeleo ya mpira wa nchi.

"Ukitazama kwa jicho pana msimamo wa ligi, unaweza kuona kuna kitu kinashtua, ukitoa wa kwanza na pili, kuanzia wa tatu hadi 16 wanaweza kushuka daraja muda wowote, ina maana ushindani upo chini na si juu. Na ushindani ukiwa chini, timu 14 zinagombania kutoshuka daraja, kutoshuka daraja ni kushindwa, kuchukua ubingwa ni kufaulu. Nilitegemea ligi ya nchi iwe na timu nyingi ziwe na timu nyingi zinagombania ubingwa, ukiona timu nyingi zinagombania kutoshuka daraja kuna walakini.

Timu nyingi zimekuwa dhaifu, tupo raundi ya 22, una timu 14 ambazo mtazamo wangu mimi kama Ahmed Ally mdau wa mpira, timu tatu pekee zimeweza kufikisha pointi 30 ambazo ni sawa na kushinda mechi 10, ambazo timu hizo zingine zimeshindwa kufanya hivyo, huwezi kusema ni ligi bora au ngumu," Ahmed alimaliza.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >